# *Hotuba Ya Ludhiana*

**Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad**
Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi
Mwanzilishi wa
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

2007
ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LIMITED

لیکچر لدھیانہ

***Hotuba Ya Ludhiana***
(Rendered into Swahili from Urdu)

© Islam International Publications Ltd.

First Swahili Edition. UK. 2007

Published by:
Islam International Publications Ltd.
'Islamabad' Sheephatch Lane,
Tilford, Surrey GU10 2AQ
United Kingdom

Printed in UK at:
Raqeem Press
Tilford, Surrey.
GU10 2AQ

ISBN: 1 85372 946 9

# MAELEZO YA MWENEZI

'Hotuba ya Ludhiana' ndiyo hotuba aliyaoitoa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad [as], Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya tarehe 4 Novemba 1905 mjini Ludhiana (India). Hotuba hiyo ilichapishwa baadaye kwa sura ya kitabu kiitwacho 'Lecture Ludhiana.'

Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya alifasiri kitabu hicho kwa Kiswahili na kwa amri ya Hadhrat Khalifatul-Masih V, Hadhrat Mirza Masroor Ahamd, Mungu Amsaidie na kumpa umri mrefu, tafsiri hii ilisahihishwa na Wabashiri hawa wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania: Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya, Sheikh Bakri Abedi Kaluta na Sheikh Ahmad Daud. Na kisha Sheikh Jamil R. Rafiq na Sheikh Bashir A. Akhtar, kwa kuagizwa na Mtukufu Khalifa walipitia mswada huu na kuusawazisha kwa kuulinganisha kwa uangalifu sana na matini ya Kiurdu. Sheikh Jamil R. Rafiq aliyekuwa Amir na Mbashiri Mkuu wa zamani wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania na Kenya, hivi sasa ni Makamu wa Mwalimu Mkuu wa Jamia Ahmadiyya Rabwah, Pakistan. Sheikh Bashir A. Akhtar aliyekuwa Amir na Mbashiri Mkuu wa zamani wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Kenya, hivi sasa anatoa huduma katika Wakalat Tasnif.

Hao wote walioshughulikia kazi hii wanastahili kushukuriwa na kuombewa. Mwenyezi Mungu na Awajaalie malipo bora.

Zingatieni kwamba maneno katika mabano ya aina hii [ ] ndiyo maelezo ya mwenezi.

Wakilut-Tasnif
Tahrik Jadid
Rabwah, Pakistan

بِسۡمِ اللّٰهِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِيۡمِ[1]

نَحۡمَدُهٗ وَ نُصَلِّی عَلٰی رَسُوۡلِهِ الۡكَرِيۡمِ[2]

# *HOTUBA YA LUDHIANA*

## *Ambayo Seyidna Ahmad[as] aliitoa mbele ya maelfu ya watu tarehe 4 Novemba 1905*

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu Aliyenipa fursa hii ya kuja tena katika mji huu kwa ajili ya kufikisha ujumbe. Nimefika mjini humu baada ya miaka 14. Niliondoka mji huu nilipokuwa na watu wachache, na hali ya kunikufurisha, kunikadhibisha na kuniita Dajjal ilikuwa imepamba moto, na machoni mwa watu nilikuwa kama mtu aliyefukuzwa na kukataliwa. Watu hao walidhani kwamba katika siku chache tu Jumuiya hii itasambaratika baada ya kukataliwa na hata jina na alama ya Jumuiya hii itafutika. Hivyo, juhudi kubwa na mipango ikafanywa kwa shabaha hii. Na njama kubwa sana ilifanywa dhidi yangu hata kwamba mimi na Jumuiya yangu ilitolewa fatuwa ya ukafiri. Na fatuwa hiyo ikatembezwa katika India nzima. Ninasikitika kusema kwamba wa kwanza kabisa kunitolea fatuwa ya ukafiri walikuwa masheikh wachache wa mji huu. Lakini mimi naona, nanyi pia mwaona kwamba walionikufurisha hawapo na Mwenyezi Mungu Ameniweka hai hadi sasa na kuiongeza Jumuiya

---

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu. [Mwenezi]

[2] Twamsifu (Yeye) na kumsalia Mtume Wake Mtukufu. [Mwenezi]

yangu. Nafikiri kwamba fatuwa ya ukafiri iliyopendekezwa mara ya pili ikatembezwa katika miji yote mikubwa ya India na ulitolewa ushahidi na kupigiwa mihuri ya maulamaa na masheikh wapatao 200. Ilielezwa humo kwamba mtu huyu hana imani, ni kafiri, ni Dajjal, ni mzushi – yu kafiri bali kafiri mkubwa kabisa. Ilmuradi, yoyote aliyoweza yeyote kusema dhidi yangu akasema. Na watu hao wakadhani kwamba silaha hii sasa itaikomesha Jumuiya hii. Kwa hakika kama Jumuiya hii ingekuwa kazi ya binadamu na uzushi, silaha hii ya fatuwa ilikuwa kali kabisa kuiangamiza. Lakini Mwenyezi Mungu ndiye Aliyeianzisha; hivyo, ingeliwezaje kuangamia kwa upinzani na uadui wa wapinzani. Kadiri upinzani ulivyozidi, vivyo hivyo adhama na heshima ya Jumuiya hii iliendelea kuimarika mioyoni. Na leo namshukuru Mwenyezi Mungu ya kwamba kulikuwa na zama nilipofika mjini humu na nikaondoka nikiwa na watu wachache tu na Jumuiya yangu ilikuwa ndogo sana. Na sasa mwaona ninayo Jumuiya kubwa pamoja nami na idadi ya wanajumuiya imekwisha fikia laki tatu na inaendelea kuogezeka siku hadi siku, na kwa yakini itafikia mabilioni.

Basi yatazameni mapinduzi haya makubwa, je hii inaweza kuwa kazi ya mkono wa kibinadamu? Watu wa dunia walitaka kufutilia mbali hata jina na alama ya Jumuiya hii. Na kama wangalikuwa na uwezo wangalikwisha ifuta tayari. Lakini hii ndiyo kazi ya Mwezyezi Mungu, na mambo Anayoyataka dunia haiwezi kuyazuia. Na mambo inayonuia dunia, ambayo Mwenyezi Mungu

Hayataki, hayawezi kutokea asilani. Fikirini! wanazuoni wote na Pirzade[3] na Gaddinashin[4] wakawa wapinzani na hata wakawafanya wafuasi wa dini nyingine waungane nao ili kunipinga. Kisha wakafanya kila juhudi dhidi yangu. Ili kuwafanya Waislamu kunidhania vibaya, wakanitolea fatuwa ya ukafiri. Waliposhindwa katika hila hiyo, basi hapo wakaanza kunishtaki mahakamani na kunishtaki katika kesi ya mauaji na kufanya kila juhudi nipate kuadhibiwa. Nikashutumiwa kwa kosa la mauaji ya padre fulani. Katika kesi hii, Sheikh Muhammad Husain pia alifanya juhudi kubwa dhidi yangu na mwenyewe akaenda kutoa ushahidi. Alitaka ninaswe na kuadhibiwa. Juhudi hii ya Sheikh Muhammad Husain ilikuwa yadhihirisha kwamba ameshindwa kuleta hoja na dalili. Na ni jambo la kawaida kwamba adui anaposhindwa kuleta dalili na asipoweza kuthibitisha tuhuma yake kwa hoja, basi hapo hutafuta njia ya kumwudhi na kumwua mwenzake na anadhamiria kumfukuza nchini na kufanya mipango na hila mbali mbali kinyume chake. Kama vile makafiri waliposhindwa mbele ya Mtume[saw] na wakawa hawana la kusema lolote, hatimaye wakafikiria hila za aina hii ya kwamba wamwue au wamfunge au afukuzwe nchini. Wakawaudhi masahaba wa Mtume[saw], lakini mwishowe wote hao wakashindwa katika hila na njama zao. Desturi na njia hiyo sasa yatumika dhidi yangu.

---

[3] Wana wa kiongozi wa kidini. [Mwenezi]
[4] Wenye kujikalia viti vya viongozi wa kidini. [Mwenezi]

Lakini dunia hii bila Mwumbaji na Mola wa walimwengu haiwezi kuwepo. Ndiye Yeye Anayepambanua baina ya mwongo na mkweli, na hatimaye Humhami mkweli na kumshindisha. Sasa katika zama hizi ambapo Mwenyezi Mungu Ameonyesha tena mfano wa kudra Yake, mimi ni ishara hai ya misaada Yake. Na sasa nyote mwaona kwamba mimi ndimi niliyekataliwa na kaumu [Waislamu]; hata hivyo ninasimama imara kama wale waliokubaliwa. Kumbukeni wakati ule nilipofika hapa miaka 14 kabla ya leo, ni nani aliyetaka niwe na hata mtu mmoja. Maulamaa, madarveshi na waheshimiwa, wote hao walitaka niangamie na jina na alama ya Jumuiya hii ifutike. Kamwe hawakupenda maendeleo yapatikane. Lakini Yule Mungu Ambaye daima Huwahami waja Wake na Aliyewashindisha wakweli, ndiye Aliyenihami. Na dhidi ya wapinzani wangu kinyume cha matarajio na mipango yao Akanijaalia nikubaliwe hata kwamba Akawaelekeza kwangu halaiki ya watu ambao wakio-ndolea mbali mapazia na vikwazo vya upinzani na matatizo, wakanijia na wanaendelea kunijia. Sasa ni jambo la kuzingatia ya kwamba je, mafanikio haya yanaweza kupatikana kwa mipango na mbinu za kibinadamu ya kwamba watu wakubwa wa dunia watafute kumwangamiza mtu na kumfanyia njama za kila aina na kumwashia moto wa hatari, lakini yeye asalimike katika maafa hayo yote. Hata kidogo. Hizi ni kazi za Mwenyezi Mungu Alizozionyesha daima.

Tena dalili kubwa ya kuthibitisha jambo hili ni kwamba miaka 25 iliyopita ambapo hata mtu mmoja hakunijua jina langu wala hakuna mtu aliyekuwa akija Qadian kunitembelea au kuwasiliana nami kwa barua, katika hali hii ya kutojulikana na katika siku hizo za kutokuwa na wasaidizi, Mwenyezi Mungu Alisema Akiniambia:

يَأْتُوْنَ مِنْ كُلِّ فَجٍّ عَمِيْقٍ وَّ يَأْتِيْكَ مِنْ كُلِّ فَجٍّ عَمِيْقٍ لَا تُصَعِّرْ لِخَلْقِ اللّٰهِ

وَ لَا تَسْئَمْ مِنَ النَّاسِ۔ رَبِّ لَا تَذَرْنِىْ فَرْدًا وَّ اَنْتَ خَيْرُ الْوَارِثِيْنَ

Hii ndiyo bishara kubwa iliyotolewa katika siku hizo na kuenezwa kwa kuchapishwa, na watu wa kila dini na taifa wakaisoma. Katika hali na wakati nilipokuwa katika upweke na mtu yeyote hakunijua, Mwenyezi Mungu Akasema kwamba watu watakujia toka nchi za mbali, nao watakuja kwa wingi na vitakuja vifaa vya kila aina na mahitaji kwa wageni hao. Kwa kuwa mtu mmoja hawezi kutosheleza mahitaji ya kuwakirimu maelfu na malaki ya watu wala hawezi kutoa gharama hizo zote, kwa hiyo Mwenyewe Akasema:

يَأْتِيْكَ مِنْ كُلِّ فَجٍّ عَمِيْقٍ

Yaani, vifaa vyao navyo vitakuja pamoja nao. Tena mtu huhangaika kuona watu wengi na hupata kuwatendea kinyume na khulka, hivyo Akakataza kwamba usiwatendee kinyume na khulka. Kisha Akasema pia ya kwamba usichoke kuona watu wengi.

Hebu fikirini sasa je, jambo hili limo katika uwezo wa

mtu kwamba miaka 25 au 30 kabla, atoe habari ya tukio fulani ambalo linamhusu yeye mwenyewe na kisha litokee vivyo hivyo? Uhai wa mtu hauwezi kutegemewa hata kwa dakika moja wala hatuwezi kusema atapumua tena au la; hivyo anawezaje kutoa habari kama hiyo kwa kubahatisha. Nasema kweli kwamba hizo zilikuwa zama nilipokuwa peke yangu kabisa na nilichukia hata kuonana na watu. Na kwa kuwa wakati ulitakiwa kuwadia kwa malaki ya watu kunielekea, hivyo kukawa na haja ya nasaha hii:

لَا تُصَعِّرْ لِخَلْقِ اللّٰهِ وَ لَا تَسْئَمْ مِنَ النَّاسِ [5]

Kisha katika siku hizo hizo Akasema:

اَنْتَ مِنِّی بِمَنْزِلَةِ تَوْحِیْدِی [6]

فَحَانَ اَنْ تُعَانَ وَ تُعْرَفَ بَیْنَ النَّاسِ

Yaani, wakati unakuja kwamba utasaidiwa na utajulikana katika watu. Kadhalika zipo funuo nyingi za Kiajemi, Kiarabu na Kiingereza zinazoeleza madhumuni hayo.

Ni jambo la kufikiria sasa kwa watu wanaomwogopa Mwenyezi Mungu kwamba bishara hiyo ilitolewa muda mrefu kabla na ikachapishwa kitabuni. Barahin-e-Ahmadiyya ni kitabu walichokisoma wote, marafiki kwa maadui; hata nakala yake moja ikapelekwa serikalini. Wakristo kwa Mabaniani walikisoma. Hata katika mji huu

---

[5] Usiwatendee viumbe wa Mungu kinyume na khulka wala usiwachoke watu [Mwenezi]

[6] Ninakupenda kama Niupendavyo Umoja Wangu. [Mwenezi]

pengine wengi wanacho kitabu hicho. Hao waangalie kwamba bishara hiyo imo ndani yake au la? Halafu masheikh ambao kwa sababu ya uadui tu wananiita Dajjal na mwongo mkubwa na wanasema kwamba bishara yoyote haikutimia, waone haya na waeleze kwamba kama hiyo siyo bishara, basi bishara yenyewe ni kitu gani? Hiki ndicho kitabu ambacho Sheikh Abu Said Muhammad Husain wa Batala amekitolea maoni yake. Kwa kuwa tulisoma pamoja, kwa hiyo mara nyingi alikuwa akija Qadian, yeye anajua vizuri, na kadhalika watu wa Qadian, Batala, Amritsar na vitongojini wanafahamu fika kuwa wakati huo nilikuwa peke yangu kabisa na kulikuwa hakuna aliyenijua. Na kutokana na hali ya wakati huo, kiakili ilikuwa haiwezekani kukisia kwamba mtu asiyejulikana kama mimi atafikiwa na zama ambapo malaki ya watu watakuwa pamoja naye. Nasema kweli kuwa wakati huo sikuwa chochote. Nilikuwa peke yangu bila msaidizi yeyote. Mwenyezi Mungu Mwenyewe katika zama hizo Akanifundisha dua hii:

رَبِّ لَا تَذَرْنِىْ فَرْدًا وَّ اَنْتَ خَيْرُ الْوَارِثِيْنَ [7]

Dua hii Akaifundisha kwa sababu Anawapenda watu wanaomwomba kwani kuomba ni ibada, maana Akasema:

اُدْعُوْنِىْٓ اَسْتَجِبْ لَكُمْ [8]

[7] Ee Mola wangu, Usiniache peke yangu na Wewe Ndiwe Mbora wa wanaorithi [Mwenezi]

[8] Al-Mu'min, 40: 61[Mwenezi]

Yaani, Niombeni, Nitakubali. Na Mtume[saw] alisema kwamba kiini cha ibada ndiyo dua. Na dokezo la pili ndani yake ni kwamba Mwenyezi Mungu kwa njia ya dua, Anataka kufundisha kuwa u peke yako, lakini wakati utafika hutabaki peke yako. Nami nasema kwa kupaza sauti kwamba kama vile mchana unavyong'aa ndivyo inavyong'aa bishara hii. Na ni kweli kwamba wakati huo nilikuwa peke yangu. Nani awezaye kuinuka na kusema kwamba ulikuwa na Jumuiya pamoja nawe? Lakini sasa tazameni kwamba sambamba na ahadi za Mwenyezi Mungu na sawa na bishara Aliyotoa Yeye zamani sana, Alinijaalia Jumuiya kubwa. Katika hali hii nani anaweza kuikadhibisha bishara hii kubwa, hususan kitabuni humo mna bishara hii pia ya kwamba, 'Watu watapinga vikali sana na watafanya jitihada ya kila aina kuizuia Jumuiya hii isiendelee. Lakini Nitawafanya washindwe.'

Aidha, ndani ya Barahin-e-Ahmadiyya mlitolewa bishara hii pia kuwa, 'Sitaacha mpaka Nipambanue mwema katika mbaya.' Siyaelezi matukio hayo kwa wale wasio na hofu ya Mwenyezi Mungu mioyoni mwao ambao kana kwamba wanajidhania hawatakufa. Hao wanageuza maneno ya Mwenyezi Mungu. Bali ninawaambia wale wanaomwogopa Mwenyezi Mungu na wana yakini kwamba watakufa na milango ya mauti inakaribia, kwani mwenye kumwogopa hawezi kukosa adabu hivyo. Hao watafakari kwamba je, kutoa bishara ya aina hii miaka 25 kabla, kunaweza kuwa matokeo ya uwezo wa kibinadamu

na kubahatisha, tena katika hali hii ambapo hakuna anayemjua, na pamoja na hayo bishara hii pia iwepo kwamba watu watapinga, lakini watashindwa. Kutabiri kushindwa kwa wapinzani na kufanikiwa kwake ni jambo lililo kinyume na kawaida. Ikiwa kuna shaka yoyote kuiamini, basi leteni mfano.

Ninasema kwa kusisitiza kwamba walete mfano wa mzushi yeyote toka Nabii Adamu[as] hadi wakakti huu ambaye katika hali yake ya kutojulikana alitoa bishara za aina hii miaka 25 kabla. Kama mtu yeyote akileta mfano wa aina hii, basi jueni kwa yakini kwamba kazi hii yote itabatilika. Lakini nani anaweza kubatilisha kazi ya Mwenyezi Mungu. Kukadhibisha hivyo na kukataa bila sababu ya kiakili na kufanya dhihaka ni kazi ya mwanaharamu; mwanahalali yeyote hawezi kujasiri hivyo. Hiyo pekee yaweza kutosha kuhakikisha ukweli wangu, kama yupo miongoni mwenu mwenye moyo mnyofu. Kumbukeni vema kwamba bishara hii haiwezi kukataliwa mpaka uletwe mfano wake. Nasema tena kwamba bishara hii imo ndani ya Barahin-e-Ahmadiyya, ambacho Sheikh Abu Said amekitolea maoni yake; pengine mjini humu Sheikh Muhammad Hasan na Munshi Muhammad Umar na wengineo watakuwa nacho. Nakala zake zilifika Makka, Madina na Bukhara. Serikali nayo ikapelekewa nakala yake. Mabaniani, Wakristo na Wabarahmu walikisoma. Sicho kitabu kisichojulikana, bali ni kitabu maarufu. Hakuna ajuaye kusoma, mwenye

tabia ya kidini asiyekijua. Tena imo bishara katika kitabu hicho kwamba 'Dunia itaungana nawe. Nitakupa umaarufu duniani na Nitawafanya wapinzani wako wasifanikiwe.' Sasa semeni je, hii inaweza kuwa kazi ya mzushi. Kama mnaamua kwamba ndiyo, hiyo yaweza kuwa kazi ya mzushi, basi ileteeni mfano. Mkileta mfano, basi nitakiri mimi ni mwongo mkubwa. Lakini hakuna awezaye kuleta mfano wake. Kama hamwezi kuleta mfano wake, na kwa yakini hamtaweza kamwe, basi nawaambieni kwamba Mwogopeni Mwenyezi Mungu na jiepusheni na kukadhibisha.

Kumbukeni kwamba si busara kuzikataa ishara za Mwenyezi Mungu bila uthibitisho wowote wala mwisho wake haujawa na baraka. Mimi sijali kukufurishwa na kukadhibishwa na yeyote wala siogopi mashambulio ninayofanyiwa; kwani Mwenyezi Mungu Mwenyewe Alikwisha niambia mapema kwamba utakadhibishwa na kukufurishwa, na watu hao watapinga vikali sana, lakini hawataweza kudhuru chochote. Je, kabla yangu wakweli na Mitume wa Mwenyezi Mungu hawakukataliwa? Ni mashambulio gani ambayo Firauni na watu wake hawakufanya dhidi ya Nabii Musa[as], mafakihi dhidi ya Nabii Isa[as] na washirikina wa Makka dhidi ya Mtume[saw]. Lakini matokeo ya mashambulio hayo yalikuwa nini? Je, wapinzani hao waliwahi kuleta mfano wowote kulingana na ishara hizi? Hata kidogo. Daima walishindwa kuleta mfano wowote. Naam, ndimi ziliendelea kupayuka, hivyo

wakadumu kuwaita waongo. Kadhalika, hapa pia waliposhindwa, hawakuweza kufanya kitu, basi wakaniita Dajjal, mwongo mkubwa. Lakini je, wataweza kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao? Hawawezi kuzima kamwe.

وَاللّٰهُ مُتِمُّ نُوْرِهٖ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُوْنَ [9]

Wale walio na tabia ya kudhania vibaya husema kuhusu miujiza na ishara nyingine huenda hiyo yote ni udanganyifu. Lakini kuhusu bishara hawawezi kuwa na udhuru wowote. Hivyo, bishara zimehesabiwa kuwa ishara kubwa zaidi na mwujiza mkubwa kabisa miongoni mwa ishara za unabii. Jambo hili limethibitika kutokana na Taurati na Kurani Tukufu pia. Hakuna mwujiza unaolingana na bishara. Hivyo Mitume wa Mwenyezi Mungu wanapaswa watambuliwe kwa bishara zao, maana Mwenyezi Mungu Amekwisha weka alama hii:

لَا يُظْهِرُ عَلٰى غَيْبِهٖ اَحَدًا اِلَّا مَنِ ارْتَضٰى مِنْ رَّسُوْلٍ [10]

Yaani, siri za Mwenyezi Mungu hazidhihiriki kwa yeyote isipokuwa kwa Mitume wateule wa Mwenyezi Mungu.

Pia ikumbukwe kwamba baadhi ya bishara zinakuwa na siri za ndani, na kwa sababu ya mambo mepesi

---

[9] Mwenyezi Mungu Atakamilisha nuru Yake ijapokuwa washirikina wachukie [Mwenezi]

[10] Al-Jinn, 72:27,28 [Mwenezi]

hazieleweki kwa wale wasio na macho ya kuonea mbali, bali wanaweza kuelewa mambo ya kawaida. Kikawaida bishara za aina hiyo hukadhibishwa , na wale wenye pupa na papara husema kuwa hazikutimia. Kuhusu hiyo, Mwenyezi Mungu Anasema:

وَظَنُّوْٓا اَنَّهُمْ قَدْ كُذِبُوْا [11]

Katika bishara hizo watu wanatia shaka, lakini kwa hakika bishara hizo hutimia sawa na sunna za Mwenyezi Mungu. Lakini hata kama hazieleweki, mwaminio na mcha-Mungu hupaswa kuziangalia bishara zisizo na mambo mepesi yaani bishara zinazoeleweka wazi. Kisha aangalie kwamba zimekwisha timia kwa wingi namna gani. Kukataa tu kwa midomo ni kinyume na ucha-Mungu. Kwa uaminifu na ucha-Mungu ziangaliwe bishara zilizokwisha timia. Lakini nani afumbe midomo ya wenye papara.

Mambo ya aina hii sikuyakabili mimi tu, bali Nabii Musa[as], Nabii Isa[as] na Mtume[saw] nao wakayakabili pia. Basi kama mimi nami nikipatwa na hali hiyo, si ajabu. Bali ilibidi ingelikuwa hivyo, maana hiyo ndiyo iliyokuwa sunna ya Mungu. Nasema kwamba kwa mwaminio hata ushahidi mmoja watosha. Kwa huo tu moyo wake hutetemeka. Lakini hapa siyo ishara moja, yapo mamia, bali ninaweza kusema kwa yakini kwamba

[11] (Makafiri) wakadhani kwamba wameambiwa uwongo.—Yusuf, 12:111
[Mwenezi]

ziko nyingi kiasi hiki kwamba siwezi hata kuzihesabu. Ushahidi huu si mdogo kwamba atazishinda nyoyo na kuwafanya wakadhibishaji waafikiane naye. Endapo mtu amwogope Mwenyezi Mungu na atafakari moyoni kwa uaminifu na busara, basi atalazimika kukubali kwamba hizo zimetoka kwa Mungu.

Tena, hili pia ni jambo lililo dhahiri kwamba mpinzani asipoibatilisha hoja wala kuleta mfano wake, hoja ya Mwenyezi Mungu ndiyo yenye kushinda.

Kwa kifupi basi, namshukuru Yule Mungu Aliyenituma. Na juu ya kuwa na shari hii na tufani iliyovuma dhidi yangu, iliyoanzia mji huu huu na kufika Delhi, Yeye Akanitoa katika tufani zote na majaribio yote salama u salimini na kunifanikisha. Na Amenileta katika mji huu katika hali hii kwamba watu zaidi ya laki tatu, wanaume kwa wanawake, wamekwisha fanya baiati yangu, na haupiti mwezi bila ya watu elfu mbili, elfu nne na pengine elfu tano kujiunga katika Jumuiya hii.

Tena, Mungu Huyo Amenisaidia wakati ambapo kaumu iligeuka kuwa adui. Wakati kaumu yenyewe ya mtu inapokuwa adui yake, basi huyo anakuwa pweke kabisa na hana la kufanya, kwani kaumu ndiyo mikono yake na miguu yake na viungo vyake, ndiyo inayomsaidia. Watu wengine huwa maadui kwa sababu anashambulia dini yao, lakini kaumu yake pia inapokuwa adui, basi hapo kusalimika na kufanikiwa si jambo dogo bali hiyo ni ishara kubwa sana.

Ninasema kwa masikitiko makubwa na uchungu wa moyo kwamba kaumu siyo tu imefanya haraka kunipinga, bali imenifanyia ukatili mkubwa pia. Kulikuwa na hitilafu katika suala moja tu la kifo cha Nabii Isa[as] ambacho nilikuwa ninathibitisha na bado nathibitisha kutoka katika Kurani Tukufu na Sunna ya Mtume[saw] na Ijmai[12] ya masahaba na dalili za kiakili na vitabu vya zamani. Na sawa na madhehebu ya Kihanafi, nilikuwa nazo dalili za kisheria — Kurani Tukufu, Hadithi na Qiyas.[13] Lakini kabla hawajaniuliza kikamilifu na kusikiliza hoja zangu, watu hao wakavuka mipaka katika kulipinga suala hili hadi nikakufurishwa. Pamoja na hayo, chochote walichotaka wakakisema na kunisingizia. Uaminifu, wema na ucha-Mungu vilihitaji kwamba wangeniuliza kwanza. Kama ningekiuka kauli ya Mwenyezi Mungu na kauli ya Mtume [saw] basi hapo bila shaka walikuwa na hiari na haki ya kuniita walivyotaka – Dajjal, mwongo mkubwa na kadhalika. Lakini tangu mwanzo nimeendelea kueleza kwamba kwenda kombo na Kurani Tukufu na ufuasi wa Mtume[saw] hata sawa na chembe naona ni kutokuwa na imani. Itikadi yangu ndiyo hii kwamba atakayeiacha hata kidogo atakwenda Motoni. Tena nimeeleza itikadi hiyo si katika hotuba tu, bali nimeibainisha kwa uwazi sana katika vitabu vyangu karibu sitini. Na iyo hiyo naifikiri na kuiwaza usiku na mchana. Basi kama

---

12 Rai za pamoja kuhusu jambo fulani la kidini huitwa Ijmai. [Mwenezi]

13 Kulinganisha jambo fulani na yale yanayofanana na hilo na kuamua huitwa Qiyas. [Mwenezi]

wapinzani hao wangemwogopa Mwenyezi Mungu, je haukuwa wajibu wao kuniuliza kwamba jambo fulani ni kinyume na Islam, sababu yake nini au unalijibuje? Lakini hapana, hawakujali hata kidogo; wakalisikia tu na kusema yu kafiri. Nakistaajabia sana kitendo chao hiki, kwa sababu suala la kifo au uhai wa Nabii Isa[as] si suala lililo sharti ya kuingia katika Islam. Hapa pia Mabaniani au Wakristo wanasilimu, lakini niambieni je, mnawalazimisha wakiri hayo isipokuwa wakiri tu:

اٰمَنْتُ بِاللّٰهِ وَ مَلَائِكَتِهٖ وَ كُتُبِهٖ وَ رُسُلِهٖ وَالْقَدْرِ خَيْرِهٖ وَ شَرِّهٖ
مِنَ اللّٰهِ تَعَالٰى وَالْبَعْثِ بَعْدَ الْمَوْتِ [14]

Kama suala hili si sehemu ya Islam, kwa nini nilipotangaza kifo cha Nabii Isa[as] nikafanyiwa ukatili kiasi hiki kwamba wafuasi wangu wakaambiwa makafiri, madajjal; wasizikwe katika mava ya Waislamu; ni halali kunyang'anya mali zao na kuwaweka wake zao kinyumba ni sawa; na kuwaua ni jambo la thawabu, na kadha wa kadha. Kulikuwa na zama ambapo masheikh hao hao walikuwa wakipiga kelele kwamba kama kuna sababu 99 za mtu kukufurishwa na sababu moja tu ya kuwa Mwislamu, hata hivyo haistahili kumtolea fatuwa ya ukafiri, mwiteni tu Mwislamu. Lakini imekuwaje sasa? Je, nimempita hata huyo katika ubaya? Je, mimi na Jumuiya yangu hatutamki shahada:

[14] Nimemwamini Mwenyezi Mungu na Malaika Wake na Vitabu Vyake na Mitume Wake na Kadri Yake ya heri na shari kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Kufufuliwa baada ya kufa [Mwenezi]

اَشْهَدُ اَنْ لَّآ اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ وَ اَشْهَدُ اَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهٗ وَ رَسُوْلُهٗ [15]

Je, mimi sisali au wafuasi wangu hawasali? Je, hatufungi saumu za Ramadhani? Na je, hatushikamani na itikadi zote alizosisitiza Mtume[saw] katika Islam?

Nasema kweli, tena nasema kwa kuapa kwa Mwenyezi Mungu ya kwamba mimi na Jumuiya yangu tu Waislamu, na Jumuiya yangu inamwamini Mtume[saw] na Kurani Tukufu kama vile Mwislamu wa kweli anavyostahili kuamini. Nina yakini kwamba kukanyaga hata hatua moja nje ya Islam ndiyo sababu ya kuangamia. Na imani yangu ndiyo hii kwamba kadiri mtu anavyoweza kupata neema na baraka na kadiri anavyoweza kupata ukaribu wa Mungu, huweza kupata tu kwa kumtii Mtume[saw] kikweli na kumpenda kikamilifu; la sivyo hapana. Hakuna njia yoyote ya wema isipokuwa yeye[saw]. Naam, hii pia ni kweli kwamba siamini kamwe kwamba Nabii Isa[as] alikwenda mbinguni akiwa hai na kiwiliwili chake na yungali hai mpaka sasa. Kwani kuamini hivyo humfedhehesha sana Mtume[saw] na kumvunjia heshima, nami siwezi kuvumilia kashfa hii hata kidogo. Wote wanajua kwamba Mtume[saw] alifariki dunia akiwa na umri wa miaka 63 na kaburi lake lipo Madina, na kila mwaka malaki ya mahujjaj pia

[15] Nashuhudia kwamba hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu na ninashuhudia kwamba Muhammad ni mtumishi Wake na Mtume Wake [Mwenezi]

wanakwenda huko. Sasa kama kuamini kifo cha Nabii Isa[as] au kumnasiblishia kifo ni kukosa adabu, basi nasema kwamba kwa nini uvunjaji huo wa heshima na kukosa adabu kumhusu Mtume[saw] kunakubaliwa? Lakini ninyi mwasema kwa furaha kubwa kwamba Mtume[saw] kafariki. Wasomaji wa Maulidi huimba kwa sauti nzuri wakieleza habari za kifo chake. Na hata mbele ya makafiri mnakiri bila kusita kwamba Mtume[saw] ameisha fariki. Sasa sielewi kwamba kifo cha Nabii Isa[as] kina shida gani kwamba mnashikwa na hasira. Hatungehuzunika kama mngetokwa na machozi kwa kusikia habari ya kifo cha Mtume[saw]. Lakini masikitiko ni kwamba mnakubali kifo cha Khataman-Nabiyyin na Mkuu wa ulimwengu kwa furaha kubwa na kumhusu yule ambaye mwenyewe anakiri kwamba hastahili hata kuilegeza gidamu ya viatu vya Mtume[saw] mnaamini yu hai, na kifo chake kikitajwa tu mnaghadhibika. Haingekuwa neno kama Mtume[saw] angekuwa hai mpaka sasa, kwa sababu alileta mwongozo wenye shani kubwa ambao mfano wake haupatikani duniani na akaonyesha zile hali kivitendo ambazo hakuna yeyote awezaye kuleta mfano wake kuanzia Adamu hadi wakati huu. Nawaambieni kwelikweli kwamba kadiri dunia na Waislamu walivyomhitaji Mtume[saw] hawakumhitaji Nabii Isa[as] kiasi hicho. Tena yu mkarimu na ndiye mwenye baraka; alipofariki hali ya masahaba ikawa kwamba walipotewa na fahamu mpaka Hadhrat Umar[ra] akatoa upanga kutoka kwenye ala yake na

akasema kwamba yeyote atakayesema kuwa Mtume[saw] amefariki nitamkata kichwa chake. Katika hali hii ya mahangaiko Mwenyezi Mungu Akamjaalia Hadhrat Abu Bakr[ra] nuru maalum na busara. Yeye aliwakusanya wote, akatoa hotuba:

مَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ ۚ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ [16]

Yaani, Muhammad (saw) ni Mtume, na Mitume waliokuja kabla yake, wote wamekwisha fariki.

Fikirini sasa na semeni kwa kutafakari kwamba kwa nini Hadhrat Abu Bakr Siddiq[ra] aliisoma aya hii alipofariki Mtume[saw] na alikuwa na makusudio na shabaha gani, hususan katika hali masahaba wote walipokuwepo? Nasema kwa yakini nanyi hamwezi kukataa kwamba mioyo ya masahaba ilishikwa na huzuni kubwa kutokana na kifo cha Mtume[saw] ambacho walikiona kimetokea wakati usiofaa na kabla ya wakati wake. Hao hawakupenda wasikie habari za kifo cha Mtume[saw] hususan katika hali ambapo sahaba mtukufu sana kama Hadhrat Umar[ra] akiwa na mahangaiko, huzuni yao kubwa isingeweza kuondoka isipokuwa aya hii ingewatuliza. Kama wangelijua au kuwa na yakini kwamba Nabii Isa[as] yungali hai, basi wangejifia papo hapo. Walikuwa wapenzi wa Mtume[saw] na wasingalivumilia uhai wa yeyote minghairi yake. Basi wangewezaje kujionea wenyewe Mtume[saw] amefariki na kuamini

[16] Aali ‘Imran, 3:145 [Mwenezi]

kwamba Nabii Isa[as] yungali hai. Ilmuradi, Hadhrat Abu Bakr[ra] alipotoa hotuba, ndipo wakatulia. Wakati huo masahaba[ra] wakawa wanasoma aya hiyo wakipita katika mitaa ya Madina, na wakafikiri kana kwamba aya hiyo imeshuka leo hii hii. Wakati huo Hassaan bin Thaabit[ra] alitunga shairi la kuomboleza ambamo alisema:

كُنْتَ السَّوَادَ لِنَاظِرِىْ فَعَمِىْ عَلَيَّ النَّاظِرُ

مَنْ شَاءَ بَعْدَكَ فَلْيَمُتْ فَعَلَيْكَ كُنْتُ اُحَاذِرُ [17]

Kwa kuwa aya iliyotajwa juu ilieleza kwamba wote wamekufa, ndiyo sababu Hassaan[ra] pia akasema kuwa sasa sijali mauti ya mtu yeyote awaye. Jueni kwa yakini kwamba baada ya Mtume[saw] kufariki, kubaki hai kwa mtu yeyote kulikuwa ni jambo zito sana kwa masahaba[ra] nao wasingaliweza kulikubali. Hivyo, wakati wa kufariki kwa Mtume[saw] hii ilikuwa Ijmai ya kwanza iliyofanyika duniani na humo suala la kifo cha Nabii Isa[as] likaamuliwa kabisa.

Mimi mara kwa mara nalitilia mkazo jambo hili kwamba dalili hii ni dalili madhubuti sana inayohakikisha kifo cha Nabii Isa[as]. Kifo cha Mtume[saw] hakikuwa jambo dogo la kawaida ambalo halingaliwahuzunisha masahaba[ra]. Afapo kiongozi wa kijiji, au mtu wa mtaani, au mtu wa nyumbani, basi watu wa nyumbani au wa mtaani au wa kijijini hupatwa na huzuni. Basi yule Nabii aliyekuja kwa dunia nzima akiwa rehema kwa walimwengu wote, kama Mwenyezi Mungu

---

[17] Ulikuwa mboni ya macho yangu, basi nimepofuka leo kwa sababu ya kifo chako. Anayetaka kufa baada yako na afe, kwani nilikuhofia wewe tu

[Mwenezi]

Alivyosema ndani ya Kurani Tukufu:

وَمَآ اَرۡسَلۡنٰكَ اِلَّا رَحۡمَةً لِّلۡعٰلَمِيۡنَ [18]

Halafu mahali pengine Akasema:

قُلۡ يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ اِنِّىۡ رَسُوۡلُ اللّٰهِ اِلَيۡكُمۡ جَمِيۡعًا [19]

Tena yule Nabii aliyeonyesha mfano wa ukweli na uaminifu na akadhihirisha sifa zisizo na kifani, haiwezekani yeye Nabii huyo afe na wafuasi wake waliojitolea kwake wasiathirike ambao hawakusita hata kidogo kumtolea mhanga uhai wao, walioziacha nchi zao, wakaacha ndugu na jamaa zao na wakaona kuvumilia kwa ajili yake taabu na shida za kila aina kuwa raha. Kwa kufikiria kidogo, jambo hili hueleweka ya kwamba uchungu na udhia walioweza kupata kwa kuwaza kifo chake, hatuwezi kukisia. Aya hiyo aliyoisoma Hadhrat Abu Bakr[ra] ndiyo iliyoweza kuwatuliza na kuwafariji. Mwenyezi Mungu Amlipe malipo mema kwa kuwaimarisha masahaba[ra] katika wakati huo mgumu.

Nasema kwa masikitiko kwamba baadhi ya wapumbavu, kwa sababu ya pupa na papara wanasema kwamba hakuna shaka Hadhrat Abu Bakr[ra] alisoma aya hii, lakini hiyo haihusikani na Nabii Isa[as]. Sijui niwaambieje wapumbavu hao! Juu ya kujiita masheikh wanaeleza maneno ya kipuuzi kama hayo. Hawaelezi

---

[18] Na Hatukukutuma ila uwe rehema kwa walimwengu wote. Al-Anbiyaa, 21:108 [Mwenezi]

[19] Sema: Enyi watu, hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu nyote.—Al-A‘raaf, 7:159. [Mwenezi]

kwamba ni neno gani katika aya hii linalomtoa nje Nabii Isa[as]. Tena, Mwenyezi Mungu Hakuliacha humo jambo lolote linalopasa kujadiliwa. Mwenyewe Akaeleza maana ya قَدْخَلَتْ [wamekwisha pita] kuwa اَفَاْئِنْ مَّاتَ اَوْ قُتِلَ [akifa au akiuawa]. Kama ingelikuwa njia nyingine ya tatu pia, kwa nini Asingalisema: اَوْ رُفِعَ بِجَسَدِهِ الْعُنْصُرِيِّ اِلَى السَّمَاءِ [au akinyanyuliwa mbinguni na kiwiliwili chake]. Je, Mwenyezi Mungu Akaishahau nao wanamkumbusha? Mungu Apishe mbali na hayo.

Kama ingekuwa aya hiyo tu, pia ingetosha. Lakini nasema kwamba hao walipenda uhai wa Mtume[saw] kiasi hiki kwamba hata leo hii watu hawa nao hulia wakikumbuka kifo chake, lakini masahaba[ra] walipata kusikia uchungu mwingi zaidi wakati huo. Nionavyo, mwaminio huwa yule anayemfuata na ndiye anayefikia daraja fulani kama Alivyosema Mwenyezi Mungu Mwenyewe:

قُلْ اِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّوْنَ اللّٰهَ فَاتَّبِعُوْنِيْ يُحْبِبْكُمُ اللّٰهُ [20]

Yaani, Sema, Kama mnampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni ili Mwenyezi Mungu Awapendeni. Sasa mapenzi hutaka kwamba mtu apende kitendo cha mpenzi wake. Na kufa ni sunna ya Mtume[saw] naye akafa. Ni nani tena ambaye abaki hai au atamani kubaki hai au amtakie mwingine kubaki hai? Mapenzi hutaka kwamba mtu ajipoteze katika ufuasi wake hivi kwamba azuie maono yake na atambue kwamba yu katika umati wa fulani. Katika hali hiyo mtu

[20] Aali'Imran, 3:32 [Mwenezi]

anayeamini kumhusu Nabii Isa[as] kwamba yungali hai hadi sasa, yeye mtu huyo anawezaje kudai kwamba anampenda na kumfuata Mtume[saw]. Maana anataka kwamba Nabii Isa[as] aboreshwe kuliko yeye[saw] naye akubaliwe kuwa maiti, lakini kwa Nabii Isa[as] anapenda akubaliwe kuwa hai.

Nasema kwelikweli kwamba kama Mtume[saw] angebaki hai, hata mtu mmoja asingebaki kafiri. Uhai wa Nabii Isa[as] umeleta matokeo gani isipokuwa wako Wakristo milioni mia nne. Hebu fikirini je, hamjaijaribu imani katika uhai wake huo na je, matokeo yake si yenye hatari? Tajeni jamii moja tu ya Waislamu ambamo kutoka humo mtu yeyote hakutanasari. Lakini naweza kusema kwa yakini kuwa jambo hili ni sawa kabisa kwamba Waislamu wa kila tabaka wamekwisha tanasari na idadi yao inaweza kuwa zaidi ya laki moja. Wakristo wanayo silaha moja tu mikononi mwao ya kuwatanasarisha Waislamu nayo ndiyo kwamba Nabii Isa[as] angali hai. Hao wanasema kwamba hakikisheni sifa hii kwa mwingine yeyote yule. Kama yeye si Mungu kwa nini basi amepewa sifa hii maalum. Yu mzima na mhifadhi wa milele. Mungu Apishe mbali na hayo. Imani hii kwamba Nabii Isa[as] yungali hai iliwajasirisha nao waliwashambulia Waislamu kwa shambulio ambalo matokeo yake nimekwisha waambieni. Sasa kinyume chake kama mkiwathibitishia mapadre kuwa Yesu amekwisha kufa, matokeo yake yatakuwaje? Nimewauliza mapadre wakubwa wakubwa nao wakasema kwamba kama

ithibitike kuwa Yesu amekufa, basi dini yetu haiwezi kubaki hai.

Kuna jambo jingine la kutafakari kwamba ninyi wenyewe mmejaribu itikadi katika uhai wa Nabii Isa[as], na sasa jaribuni kidogo imani katika kifo chake na angalieni kwamba dini ya Kikristo inapata pigo gani kwa imani hii. Popote mfuasi wangu anapozungumza na Wakristo juu ya habari hii, mara moja hukataa kuzungumza kwa sababu wanajua kuwa kwa njia hii maangamio yao yapo karibu. Kwa imani katika kifo, haiwezi kuthibitika kafara ya Yesu wala uungu wake wala yeye kuwa mwana wa Mungu. Basi jaribuni imani hii kwa siku chache, ndipo uhakika wenyewe utakuwa wazi.

Sikilizeni, ndani ya Kurani Tukufu na Hadithi za Mtume[saw] kulikuwa na ahadi kwamba Islam itaenea na itazishinda dini nyingine na msalaba utavunjika. Jambo la kufikiria sasa ni hili kwamba duniani njia huhitajika kufanya kila jambo. Mtu auguapo hakuna shaka kwamba Mwenyezi Mungu ndiye Anayeponya, lakini kwa ajili yake Yeye ndiye Alitia sifa katika dawa. Mtu anapopewa dawa yamnufaisha. Asikiapo kiu Aizimaye ndiye Mungu, lakini Yeye ndiye Aliyeweka maji pia kwa shabaha hiyo. Halikadhalika, asikiapo njaa, ndiye Yeye Anayeiondoa, lakini ndiye Aliyeweka chakula pia. Vivyo hivyo, ushindi wa Islam na uvunjaji wa msalaba utatokea jinsi Alivyokadiria, lakini kwa shabaha hiyo Yeye ndiye Aliyeziweka njia na kuweka kanuni moja. Hivyo, jambo

hili limekubaliwa kwa kauli moja sawa na Kurani Tukufu na Hadithi kuwa katika zama za mwisho ambapo Ukristo utakuwa na ushindi, Islam itashinda kwa njia ya Masihi Aliyeahidiwa naye ataishindisha Islam juu ya dini na mila zote na atamwua Dajjal na kuvunja msalaba, na zama zile zitakuwa zama za mwisho. Nawwab Siddiq Hasan Khan na waja wengine walioandika vitabu kuhusu zama za mwisho nao wamelikubali jambo hili. Sasa kwa kutimia bishara hiyo kutakuwa na sababu na njia pia, maana ni desturi ya Mwenyezi Mungu kwamba Yeye Hutumia njia. Huponya kwa dawa na kwa vyakula na maji Huondoa njaa na kiu. Sasa kwa vile ushindi wa dini ya Kikristo umekwisha tokea na Wiaslamu wa kila tabaka wamekwisha ingia katika kundi hilo, Mwenyezi Mungu Amekusudia kuishindisha Islam sawa na ahadi Yake. Kwa shabaha hiyo kutakuwa na njia na sababu kwa vyovyote, na hiyo ndiyo silaha ya kifo cha Nabii Isa[as] na kwa silaha hiyo dini ya msalaba itajifia na wataishiwa nguvu. Nasema kwelikweli kwamba kwa kuondoa makosa ya Wakristo ni njia gani inayoweza kuwa kubwa zaidi kuliko kuthibitisha kifo cha Nabii Isa[as]. Tafakarini jambo hili mkiwa nyumbani mwenu na fikirini mlalapo faraghani vitandani. Katika hali ya upinzani mtu hushikwa na harara, lakini mwenye tabia njema hufikiria. Nilipotoa hotuba huko Delhi, watu wenye tabia njema walikubali na papo hapo wakatamka kwamba bila shaka nguzo ya Nabii Isa[as] kuabudiwa ni imani katika uhai

wake; isipovunjika hii, mlango haufunguki kwa ajili ya Islam, bali hiyo husaidia Ukristo.

Wale waupendao uhai wake wanapaswa wafikirie kwamba kwa ushahidi wa mashahidi wawili mtu hunyongwa, lakini hapa kuna ushahidi mwingi sana nao wanaendelea kukataa. Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Kurani Tukufu:

يٰعِيۡسٰٓى اِنِّىۡ مُتَوَفِّيۡكَ وَرَافِعُكَ اِلَىَّ [21]

Tena kukiri kwa Nabii Isa[as] mwenyewe kunapatikana ndani ya Kurani hii hii:

فَلَمَّا تَوَفَّيۡتَنِىۡ كُنۡتَ اَنۡتَ الرَّقِيۡبَ عَلَيۡهِمۡ [22]

Na maana ya 'tawaffii' kuwa kifo huthibitika katika Kurani Tukufu, kwa sababu neno hilo limetumika kwa ajili ya Mtume[saw] pia kama Alivyosema:

وَاِمَّا نُرِيَنَّكَ بَعۡضَ الَّذِىۡ نَعِدُهُمۡ اَوۡ نَتَوَفَّيَنَّكَ [23]

Na Mtume[saw] amesema فَلَمَّا تَوَفَّيۡتَنِىۡ ambayo maana yake ni kifo tu. Halikadhalika, neno hilo limetumika kwa Nabii Yusuf [as] na watu wengine pia. Basi katika hali hiyo linawezaje kuwa na maana nyingine? Huu ndio ushahidi mkubwa sana juu ya kifo cha Nabii Isa[as]. Zaidi ya hayo, katika usiku wa Mi'raaj Mtume[saw] alimwona Nabii Isa[as]

---

[21] Ewe Isa, kwa yakini Mimi Nitakufisha, na Nitakuinua Kwangu. Aali'Imraan, 3:56 [Mwenezi]

[22] Uliponifisha Wewe Ukawa Mchungaji juu yao.—Al-Maaida, 5:118 [Mwenezi]

[23] Na kama Tukikuonyesha baadhi ya yale Tunayowaonya au Tukufishe. Yunus, 10:47 [Mwenezi]

akiwa miongoni mwa wafu. Hakuna yeyote awezaye kukataa Hadithi ya Mi'raaj. Iangalieni hiyo je, humo Nabii Isa[as] ametajwa akiwa pamoja na wafu ama kwa njia nyingine. Jinsi alivyowaona Nabii Ibrahimu[as], Nabii Musa[as] na Manabii wengine, ndivyo alivyomwona Nabii Isa[as]. Kulikuwa hamna tofauti yoyote baina yao. Hakuna anayeweza kukataa kwamba Nabii Musa[as] na Nabii Ibrahimu[as] na Manabii wengine wamekwisha fariki na Malaika mwenye kuchukua roho amewafikisha katika ulimwengu mwingine. Basi mtu mmoja kati yao amekwendaje akiwa hai na mwili wake? Shuhuda hizi si chache; zamtosha Mwislamu wa kweli.

Tena katika Hadithi nyingine umri wa Nabii Isa[as] umetajwa kuwa miaka 120 au 125. Baada ya kuyaangalia mambo hayo yote kwa pamoja ilikuwa kinyume na ucha-Mungu kutoa uamuzi haraka kuwa Nabii Isa[as] akiwa hai amekwenda mbinguni na tena hakuna mfano wake. Akili pia ilitaka hivyo, lakini inasikitisha kwamba watu hao hawakujali hata kidogo, na bila kumwogopa Mungu haraka sana wakaniita Dajjal. Fikirini je, hili lilikuwa jambo dogo? Ni masikitiko!

Tena inaposhindikana kutoa udhuru wowote husema kwamba katika zama za kati Ijmai imekwisha fanyika. Nasema lini? Ijmai ya kweli ilikuwa Ijmai ya masahaba[ra]. Kama Ijmai ilifanyika baadaye, basi yaunganisheni pamoja madhehebu hayo mbalimbali. Nasema kweli kwamba hii si sawa hata kidogo. Uhai wa Nabii Isa[as] haukufanyiwa Ijmai wakati wowote. Hao hawakusoma

vitabu, la sivyo wangejua kwamba masufi wana imani katika kifo cha Nabii Isa[as] nao wanaamini ujaji wake wa mara ya pili ni kwa njia ya 'Buruuz' (mfano).
Ilmuradi, kama vile nilivyomhimidia Mwenyezi Mungu, ndivyo ninavyomsalia Mtume[saw] kwamba Mwenyezi Mungu Ameanzisha Jumuiya hii kwa ajili yake tu na misaada hii inaendelea kupatikana kwa sababu ya neema na baraka zake. Nasema kwa uwazi kabisa nayo ndiyo itikadi yangu na imani yangu kwamba bila kumfuata Mtume[saw] na kukanyaga katika nyayo zake mtu yeyote hawezi kupata neema yoyote ya kiroho na fadhili.

Pamoja na hayo, kuna jambo jingine linalopasa kutajwa, nisipolitaja itakuwa ni utovu wa shukrani, nalo ni kwamba Mwenyezi Mungu Ametuumba katika utawala na serikali inayotoa amani ya kila aina na ambayo imetupatia uhuru kamili wa kuhubiri na kueneza dini yetu, na tunazo nyenzo za kila aina katika enzi hii yenye baraka. Uhuru gani waweza kuwa zaidi ya huu kwamba tunaibatilisha dini ya Kikristo kwa nguvu sana na hakuna anayetuzuia. Lakini hapo kabla kulikuwa na zama, na waliozipata hizo zama wapo mpaka sasa; wakati huo hali ilikuwa kwamba Waislamu hawakuweza hata kutoa adhana ndani ya misikiti yao. Achilia mbali mambo mengine, hata vitu vilivyo halali vilikataliwa kuliwa. Uchunguzi wowote ulikuwa haufanywi. Lakini ni fadhili na hisani ya Mwenyezi Mungu kwamba tupo chini ya serikali iliyoepukana na aibu hizo zote. Yaani serikali ya

Kiingereza inayopenda amani, ambayo haijali hitilafu za dini, ambayo sheria yake ni kwamba wafuasi wa kila dini watekeleze wajibu wao kwa uhuru. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu Amekusudia kwamba mahubiri yetu yafike kila mahali, ndiyo sababu Ametuumba katika serikali hii. Kama Mtume[saw] alivyokuwa akionea fahari enzi ya Naushirwan, ndivyo tunavyoionea fahari serikali hii. Ni jambo la kawaida kwamba kwa kuwa Mtume huleta uadilifu na ukweli, kwa hiyo kabla hajatumwa yeye, uadilifu na ukweli huanza kupatikana. Mimi nina yakini kwamba serikali hii ni bora sana na afadhali kuliko serikali ya Kirumi iliyokuwepo katika zama za Nabii Isa[as]. Ingawa sheria zao zinafanana, lakini uadilifu ndio huu kwamba sheria za serikali hii hazishindikani mbele ya mtu yeyote na zikilinganishwa na zile za Kirumi itajulikana kwamba katika serikali ya Kirumi lazima kulikuwa na kiasi fulani cha ukatili. Lakini huu ulikuwa woga kwamba kwa kuwaogopa Mayahudi, mja mtakatifu na mteule wa Mungu, Nabii Isa[as] akawekwa kifungoni. Mimi pia nilifanyiwa kesi ya aina hii. Waliomshtaki Nabii Isa[as] walikuwa Mayahudi, lakini aliyenishtaki katika serikali hii alikuwa padre mwenye heshima na pia alikuwa daktari, yaani Dkt. Martin Clark, ndiye aliyenishtaki kwamba nilipanga kumwua na akaandaa ushahidi kamili hata kwamba Sheikh Abu Said Muhammad Husain wa Batala aliye adui mkali wa Jumuiya hii, naye akafika mahakamani kwa kutoa ushahidi. Na kadiri

alivyoweza akatoa ushahidi dhidi yangu na akajitahidi kikamilifu kuthibitisha mashtaka dhidi yangu. Kesi hiyo ilisikilizwa na Mkuu wa wilaya wa Gurdaspur, Kapteni Douglas, ambaye nadhani sasa yuko Simla. Kesi ikasikilizwa naye kikamilifu na ushahidi wote dhidi yangu ulitolewa kwa nguvu zote. Katika hali hii hata mwanasheria yeyote mahiri hangeweza kusema kwamba naweza kuachiliwa huru. Hali zilivyotokea zilitaka kwamba ningepelekwa mahakama ya juu na huko ningehukumiwa kunyongwa au kupatiwa adhabu ya kufukuzwa nchini. Lakini kama vile Mwenyezi Mungu Alivyonipasha habari kabla ya kesi hiyo, ndivyo Alivyoniambia mapema kwamba nitaachiliwa. Basi kundi kubwa la wafuasi wangu walijua bishara hii. Ilmuradi, kesi ilipofikia hatua hii na maadui na wapinzani wakadhani kwamba sasa hakimu atanipeleka mahakama ya juu, hapo yeye akamwambia Mkuu wa Polisi kuwa inanijia moyoni kwamba kesi hii ni ya kubuniwa. Moyo wangu hauamini kama kweli jaribio hili lilifanywa na akatumwa mtu kwenda kumwua Dkt. Clark; hivyo uichunguze tena. Huo ulikuwa ni wakati ambapo siyo tu kwamba wapinzani wangu walishughulikia njama za kila aina dhidi yangu, bali watu waliodai kwamba hupokelewa maombi yao, wakashughulikia kuomba wakilia machozi nipate kuadhibiwa. Lakini ni nani awezaye kushindana na Mwenyezi Mungu? Ninajua kwamba Kapteni Douglas alishauriwa na baadhi ya watu niadhibiwe, lakini yeye alikuwa hakimu mpenda uadilifu, akasema

kwamba hatuwezi kuwa na ushenzi namna hii.
Ilmuradi, kesi hii alipokabidhiwa Kapteni Le Marchand kwa ajili ya upelelezi mara ya pili, basi Kapteni akamwita Abdul Hamid na kumwambia, 'Sema kweli tupu.' Hapo tena Abdul Hamid akarudia kisa kile kile alichosimulia mbele ya Mkuu wa wilaya. Mwanzoni kabisa aliambiwa na Wakristo kwamba kama ukieleza kinyume hata kidogo na maelezo yako ya awali, utashikwa; hivyo akasema yale yale. Lakini Kapteni akamwambia kwamba, 'Umekwisha sema hayo awali, lakini Bwana mkubwa haridhiki nayo kwa sababu wewe husemi kweli.' Kapteni Le Marchand alipomwambia mara ya pili, akamwangukia miguuni, huku akilia na kusema, 'Niokoe.' Kapteni akamtuliza na kusema, 'Ndiyo, eleza'. Hapo yeye akatoboa ukweli na akakiri kwa uwazi kabisa kwamba, 'Nililazimishwa kueleza kwa kutishwa; kamwe kabisa Bwana Mirza hakunituma kuua.' Kapteni alifurahi sana kusikia maelezo hayo na akampigia simu Mkuu wa wilaya kwamba tumekwisha pata uhakika wa kesi. Basi kesi hiyo ikasikilizwa tena mjini Gurdaspur, na Kapteni Le Marchand aliapishwa naye akaandikisha maelezo yake kwa kuapa. Niliona kwamba Mkuu wa wilaya alifurahi mno kwa kudhihirika ukweli na akawakasirikia sana wale Wakristo waliotoa ushahidi wa uwongo dhidi yangu. Akaniambia: 'Unaweza kuwashtaki Wakristo hao.' Lakini kwa kuwa mimi nachukia kushtakiana, hivyo nikamwambia kwamba: 'Sipendi kushtaki; kesi yangu inaendelea

huko mbinguni.' Papo hapo Bwana Douglas akaandika hukumu. Watu wengi walijumuika siku hiyo. Akitoa hukumu akaniambia. 'Hongera, umeachiliwa.'

Sasa semeni ni sifa nzuri ilioje ya serikali hii kwamba kwa ajili ya uadilifu haikujali hata kiongozi wa dini yake wala kitu kingine chochote. Wakati huo niliona dunia nzima ilikuwa adui yangu. Na ndivyo inavyokuwa kwamba dunia inaponuia kumtesa mtu, kila kitu humwudhi. Ni Mwenyezi Mungu tu pekee Anayewaokoa watumishi Wake wa kweli.

Tena nilishtakiwa mbele ya Bwana Dowie. Kisha nikazuliwa kesi ya kodi. Lakini katika kesi hizo zote Mwenyezi Mungu Akadhihirisha sina hatia. Hatimaye kukawa kesi ya Karam Din. Katika kesi hii nguvu zote zikatumiwa dhidi yangu na ikadhaniwa kwamba sasa basi huu ndio mwisho wa Jumuiya hii. Kwa hakika kama Jumuiya hii isingetoka kwa Mwenyezi Mungu na Yeye Mwenyewe Asingeisaidia na kuinusuru, basi kusingekuwa na shaka yoyote katika kufutika kwake. Karam Din akaungwa mkono na watu toka pembe moja ya nchi hadi pembe ya pili na akasaidiwa kwa kila njia hata kwamba katika kesi hiyo baadhi ya wale wanaojiita masheikh wakatoa ushahidi wa uwongo dhidi yangu na wakasema hata kama yu [Karam Din] mzinzi, fasiki, mpujufu, hata hivyo yu mcha-Mungu. Kesi hii iliendelea kwa muda mrefu. Katika muda huo ishara nyingi zilidhihirika. Mwishowe hakimu aliyekuwa Baniani

akanitoza faini rupia mia tano. Lakini Mwenyezi Mungu tangu awali Alinipasha habari kwamba 'Mahakama ya juu imemwachilia'. Hivyo, rufaa ilipopelekwa mbele ya jaji wa Division,[24] kwa busara aliyopewa na Mungu, mara moja akafahamu uhakika wa kesi na kusema kwamba niliyoandika mimi kumhusu Karam Din yalikuwa sawa kabisa, yaani nilikuwa na haki ya kuyaandika. Basi hukumu aliyoiandika imekwisha chapwa. Hatimaye, akaniachilia, akanirudishia faini na akaikemea ipasavyo mahakama ya mwanzo kwamba kwa nini kesi hiyo imecheleweshwa kwa muda mrefu.

Ilmuradi, kila wapinzani wangu walipopata nafasi wakafanya chini juu kuniponda na kuangamiza, lakini Mwenyezi Mungu kwa fadhili Zake tu Akaniokoa katika kila moto kama vile ambavyo Aliendelea kuwaokoa Mitume Wake. Nikiangalia matukio hayo nasema kwa nguvu kabisa kwamba serikali hii ni bora zaidi kuliko serikali ya Kirumi ambayo katika enzi yake Nabii Isa[as] aliteswa. Gavana Pilato ambaye kwanza kesi ilipelekwa mbele yake, kwa hakika alikuwa mfuasi wa Nabii Isa[as] na mkewe naye alikuwa mfuasi. Ndiyo sababu akanawa mikono yaka kwamba hana hatia katika damu ya Yesu. Lakini ingawa alikuwa mfuasi tena Gavana, hakuwa na ushujaa aliouonyesha Kapteni Douglas. Huko Yesu hakuwa na hatia na hapa mimi sikuwa na hatia.

---

24 Eneo kubwa kuliko wilaya lakini dogo kuliko mkoa. [Mwenezi]

Nasema kwelikweli tena kwa kujaribu kwamba Mwenyezi Mungu Amewapa watu hao ushujaa kwa ajili ya haki. Hivyo, nawasihi hapa Waislamu kwamba wanawajibika kutii serikali hii kwa moyo wa kweli.

Kumbukeni vema kwamba asiyemshukuru mhisani wake hawezi kumshukuru Mwenyezi Mungu. Raha na starehe zinazopatikana katika zama hizi hazina kifani. Angalieni mifumo ya reli, simu, posta, polisi n.k. kwamba faida nyingi namna gani hupatikana kwayo. Je, zilikuwapo raha hizo na starehe miaka sitini au sabini hapo kabla? Basi semeni kwa haki kwamba kwa nini tusitoe shukrani ilhali tunafanyiwa maelfu ya hisani. Waislamu wengi wananishambulia kwa kusema kwamba Jumuiya yako ina ubaya huu kwamba mnatangua Jihadi. Ni masikitiko kwamba wajinga hao hawaelewi kabisa uhakika wake. Wanaikashifu Islam na Mtume[saw]. Kamwe hakunyanyua upanga kwa kueneza dini. Dhuluma za wapinzani juu ya Mtume[saw] na wafuasi wake zilipofikia kikomo na miongoni mwa wafuasi wake waaminifu wanaume kwa wanawake wakauawa na kisha akafuatwa hadi Madina, ndipo akapata amri ya kupambana nao. Yeye hakuinua upanga kwanza, bali maadui ndio waliuinua. Wakati mwingine makafiri wadhalimu walimjeruhi mwili mzima hata akatokwa na damu kichwani mpaka miguuni, hata hivyo hakupambana nao. Kumbukeni vizuri kwamba kama kutumia upanga kungekuwa ni faradhi katika Islam, basi Mtume[saw]

angeunyanyua huko Makka, lakini sivyo. Upanga unaozungumziwa ukainuliwa wakati makafiri wenye kuudhi walipomfuata hadi Madina. Wakati huo wapinzani walikuwa na upanga mikononi mwao. Lakini sasa upanga hakuna, bali wanatumia dhidi yangu habari za uwongo na fatuwa, na ni kalamu tu inayotumika kuipinga Islam. Hivyo, mwenye kuijibu kalamu kwa upanga si atakuwa mpumbavu na mjinga, ama nani?

Msisahau kwamba Mtume[saw] aliinua upanga baada ya makafiri kupita kiasi katika dhuluma na ukatili, na hii ilikuwa ni hatua ya kujilinda ambayo katika sheria ya kila serikali iliyostaarabika inajuzu. Kama mwizi akiingia nyumbani naye anashambalia kwa nia ya kuua, wakati huo kumwua mwizi huyo kwa kujiokoa si hatia.

Hivyo hali ilipofikia kiasi hiki kwamba wafuasi waaminifu wa Mtume[saw] waliuawa hata wanawake dhaifu wa Kiislamu nao wakauawa kwa ukatili na bila kuona haya, je haikuwa haki kwamba hao [maadui] waadhibiwe? Wakati huo kama Mwenyezi Mungu Angekusudia kwamba jina la Islam lisibaki, hapo upanga usingeliweza kuinuliwa. Lakini Alitaka Islam ienee duniani na iwe njia ya wokovu wa dunia, ndiyo maana wakati huo upanga uliinuliwa kwa kujilinda tu. Nasema kwa kusisitiza kwamba wakati huo Islam kunyanyua upanga si jambo la kulaumiwa sawa na kanuni na dini yoyote na khulka. Watu wanaofundisha kwamba 'ukipigwa shavu moja, geuza na la pili,' hawawezi

kusubiri, na wale ambao wanaona hata kumwua mdudu ni dhambi nao hawawezi kuvumilia. Sasa kwa nini Islam inalaumiwa?

Nasema pia kwa uwazi kwamba Waislamu majahili wasemao kwamba Islam ilienea kwa upanga, wanamzulia uwongo Nabii Maasumu na wanaivunjia Islam heshima. Kumbukeni vema kwamba Islam daima imeenea kwa sababu ya mafundisho yake matakatifu na mwongozo na kwa nuru na baraka na miujiza yake. Ishara kubwa za Mtume[saw] na athari tukufu za khulka zake njema zimeieneza, na ishara na athari hizo bado hazijaisha bali huwepo katika kila zama bila kufifia. Ndiyo sababu nasema kwamba Mtume wetu[saw] ni Nabii aliye hai, kwani mafundisho yake na maagizo yake daima hutoa matunda yake, na katika siku zijazo Islam itakapopata maendeleo, basi hiyo ndiyo itakuwa njia yake, si nyingine. Kwa kuwa upanga haukutumika wakati wowote kwa kueneza Islam, hivyo kuliwaza hilo wakati huu ni dhambi. Maana wote wanaishi kwa amani na kwa ajili ya kueneza dini yao ziko njia na nyenzo za kutosha.

Nasikitika sana kusema kwamba Wakristo na wapinzani wengine wakati wa kushambulia Islam hawakutafakari kamwe uhakika wenyewe. Walipaswa kuona kwamba wapinzani wote wakati huo walijitokeza kuing'olea mbali Islam na Waislamu na wote kwa pamoja wakala njama dhidi yake na kuwatesa Waislamu. Kukabiliana na mateso na udhia, kama wasingelijilinda

wangelifanyeje? Ndani ya Kurani Tukufu kuna aya hii:

أُذِنَ لِلَّذِيْنَ يُقَاتَلُوْنَ بِأَنَّهُمْ ظُلِمُوْا [25]

Hii yaonyesha kwamba agizo hili lilitolewa ambapo dhuluma dhidi ya Waislamu ilifikia kikomo, ndipo amri ya kupambana ikatolewa. Ruhusa hii ilikuwa kwa wakati huo, siyo kwa wakati mwingine. Basi Masihi Aliyeahidiwa aliwekewa alama hii :[26] يَضَعُ الْحَرْبَ Sasa, basi, alama ya ukweli wake ni kwamba hatapigana vita. Sababu yake ndiyo hii kwamba katika zama hizi wapinzani nao wameacha vita vya kidini. Naam, mashindano haya yamechukua sura nyingine, nayo ni kwamba wanaipinga Islam kwa kutumia kalamu. Ama Wakristo, kila gazeti lao hutolewa nakala elfu hamsini na wanajitahidi kwa kila namna kwamba watu waichukie Islam. Kwa ajili ya mashindano haya, yatupasa tutumie kalamu au tupige mishale? Kama mtu akifikiria hivyo, ni nani atakayekuwa mpumbavu mkubwa na adui wa Islam kuliko yeye? Kusema tu hivyo ni kuaibisha Islam ama nini? Wapinzani wetu wasipofanya juhudi ya aina hii, ilhali hawako juu ya haki, basi itakuwa ajabu na la kusikitisha kwamba sisi tulio juu ya haki tutaje upanga. Wakati huu umwonyeshe mtu upanga na kumwambia 'Silimu au la nitakuua,' halafu uone

---

[25] Imeruhusiwa kupigana kwa wale wanaopigwa, kwa sababu wamedhulumiwa.—Al-Hajj, 22:40 [Mwenezi]

[26] Ataiondoa vita [Mwenezi]

matokeo yatakuwaje? Yeye atakufanya ukamatwe na polisi na kukuonjesha ladha ya upanga.

Mawazo haya ni ya kipuuzi kabisa na yanatakiwa yaondolewe vichwani. Sasa wakati umefika kwamba uonyeshwe uso wenye nuru na mng'aao wa Islam. Hizi ni zama za upinzani wote kufutiliwa mbali na doa lililotiliwa kwenye uso mng'aao wa Islam kuondolewa kabisa. Nasikitika kusema kwamba fursa ambayo Mwenyezi Mungu Amewajaalia Waislamu na njia iliyofunguliwa kwa Wakristo kuingia Islam, wakaiona vibaya na kuikataa.

Kwa njia ya maandiko yangu, nimeeleza njia itakayoifanikisha na kuishindisha Islam juu ya dini nyingine. Majarida yangu yanafika Amerika na Ulaya na kwa sababu ya busara ambayo Mwenyezi Mungu Amewajaalia watu hawa, wamelifahamu jambo hili. Lakini ninapomweleza Mwislamu njia hiyo, basi povu hutoka kinywani mwake kana kwamba yu mwehu ama ataka kuua, ilhali fundisho la Kurani Tukufu ndilo hili:

اِدْفَعْ بِالَّتِیْ هِیَ اَحْسَنُ [27]

Shabaha ya fundisho hili ilikuwa ni kwamba hata kama ni adui, kwa upole na wema huu ageuke kuwa rafiki na asikilize maneno haya kwa utulivu na usikivu. Ninasema kwa kuapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba mimi nimetoka Kwake. Yeye Anajua sana kwamba mimi si

[27] Zuia ubaya kwa yaliyo mema zaidi.—Haa Miim As-Sajda, 41:35
[Mwenezi]

mzushi, si mwongo. Ikiwa ninyi baada ya mimi kuapa kwa Mwenyezi Mungu na pia kuziona ishara ambazo Yeye Amedhihirisha kunisaidia, bado mnaniita mwongo na mzushi, basi nawaombeni kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba leteni mfano wa mzushi yeyote ambaye juu ya kumzulia Mwenyezi Mungu na kumwongopea kila siku, Mungu Aendelee kumsaidia na kumnusuru. Ilitakiwa Amwangamize, lakini hapa mambo ni kinyume chake. Nasema kwa kula kiapo cha Mwenyezi Mungu kwamba mimi ni mkweli na nimetoka Kwake, lakini naitwa mwongo na mzushi. Tena Mwenyezi Mungu katika kila kesi na kila balaa wanayozusha watu dhidi yangu, Hunisaidia na kuniokoa. Na Akanisaidia hivi kwamba Akawatilia malaki ya watu mapenzi yangu mioyoni mwao. Hii inatosha kuhakikisha ukweli wangu. Kama mkiweza kumtaja mzushi aliye mwongo na akamzulia Mwenyezi Mungu uwongo na Mwenyezi Mungu Akamsaidia hivyo na kumweka hai kwa muda huo na kumtimizia matamanio yake, nionyesheni basi.

Fahamuni kabisa kwamba Mitume wa Mwenyezi Mungu hutambulikana kwa ishara ambazo Mwenyezi Mungu Huzionyesha kwa ajili yao na kuwasaidia. Mimi ni mkweli katika usemi wangu na Mwenyezi Mungu Aionaye mioyo Anajua habari ya moyo wangu na kuitambua. Je, hamwezi hata kusema

yale aliyoyasema mmojawapo wa watu wa Firauni:

اِنْ يَّكُ كَاذِبًا فَعَلَيْهِ كَذِبُهٗ

وَاِنْ يَّكُ صَادِقًا يُّصِبْكُمْ بَعْضُ الَّذِىْ يَعِدُكُمْ [28]

Je, hamna yakini kuwa Mwenyezi Mungu ni adui mkubwa kabisa wa waongo. Ghadhabu ya Mwenyezi Mungu inakuwa kali zaidi kuliko ninyi nyote kunishambulia pamoja. Basi ni nani awezaye kuokoa katika ghadhabu Yake. Na aya ambayo nimeitaja ina jambo linalostahili kukumbukwa kwamba Atatimiza baadhi ya bishara za maonyo, si zote. Humo mna hekima gani? Hekima ndiyo hii kwamba bishara za maonyo huwa na masharti na hutanguka kwa kutubu na kuomba ghofira na kurejea kwenye haki.

Bishara huwa ya aina mbili. Kwanza ya ahadi, Alivyosema:

وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ [29]

Ahli Sunna wanaamini kwamba bishara za aina hii hazitanguki, kwani Mwenyezi Mungu ni Karimu. Ama bishara za maonyo, pengine baada ya kuonya Anasamehe kwa sababu Yu Rahimu. Ni mjinga sana na mbali na Islam anayesema kwamba bishara zote za maonyo hutimia. Huyo anaiacha Kurani Tukufu, kwa sababu

---

[28] Akiwa mwongo, basi uwongo wake ni juu yake, na kama yu mkweli, yatawafikieni baadhi ya hayo anayowaonyeni.—Al-Mu'min, 40:29 [Mwenezi]

[29] Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu. An-Nur, 24:56 [Mwenezi]

Kurani Tukufu yasema:

يُصِبْكُمْ بَعْضُ الَّذِىْ يَعِدُكُمْ [30]

Inasikitisha kwamba watu wengi wanajiita mashiekh lakini hawajui Kurani wala Hadithi wala sunna ya Manabii. Huwa povu tu la bughudha, hivyo wanadanganya. Kumbukeni:

اَلْكَرِيْمُ اِذَا وَعَدَ وَفٰى [31]

Rahimu huwa Anamsamehe mtu baada ya kumhukumu kuadhibiwa. Na hii ni tabia ya mtu pia kwamba anasamehe. Safari moja, mtu fulani alitoa ushahidi wa uwongo mbele yangu ambaye ilithibitika ana hatia. Kesi hii ikasikilizwa na hakimu mmoja Mwingereza. Kwa bahati akapata barua ya kwamba amehamishwa mahali pa mbali sana. Akahuzunika kwani yule mwenye hatia alikuwa mzee. Akamwambia karani, 'Huyo atafia jela tu.' Karani naye akasema, 'Bwana! huyo ana watoto.' Hapo yule Mwingereza akasema, 'Sasa faili imekwisha kamilika, yaweza kufanywa nini sasa.' Halafu akasema, 'Haya, ichane faili hii.' Sasa tafakarini, Mwingereza anaweza kuwa na huruma, kwa nini Mwenyezi Mungu Hawezi.

Tena fikirini pia kwamba kwa nini sadaka hutolewa, na kila kaumu ina desturi hii. Kitabia mtu hupenda kutoa

---

[30] Yatawafikieni baadhi ya hayo anayowaonyeni.—Al-Mu'min, 40:29 [Mwenezi]

[31] Mkarimu anapoahidi hutimiza [Mwenezi]

sadaka wakati wa msiba na balaa na huitoa pia. Wanasema, 'Toa mbuzi, toa nguo, toa hiki, toa kile.' Ikiwa balaa haliondoki kwa njia hii, kwa nini mtu hulazimika kufanya hivi. Hapana, balaa huondoka. Jambo hili limethibitika kwa kuafikiwa na Mitume laki moja elfu ishirini na nne. Nami najua kwa yakini kwamba hii siyo imani ya Waislamu tu, bali pia ni imani ya Wayahudi, Wakristo na Mabaniani. Na ninavyofahamu hakuna yeyote duniani anayekataa jambo hili. Kama ni hivyo, basi imedhihirika kwa uwazi kabisa kwamba dhamira ya Mungu hutanguka.

Tofauti kati ya bishara na dhamira ya Mungu ni hii tu kwamba habari ya bishara hupewa Nabii, lakini dhamira ya Mungu hafahamishwi yeyote nayo hubaki siri. Kama dhamira hiyo ya Mungu ingedhihirishwa kwa njia ya Nabii, ingekuwa bishara. Kama bishara haiwezi kutanguka, basi dhamira ya Mungu pia haiwezi kutanguka kwa sadaka. Lakini hii si sawa hata kidogo. Kwa kuwa bishara za maonyo hutanguka, ndiyo maana Akasema:

وَاِنْ يَّكُ صَادِقًا يُّصِبْكُمْ بَعْضُ الَّذِىْ يَعِدُكُمْ [32]

Sasa Mwenyezi Mungu Mwenyewe Anatoa ushahidi kwamba baadhi ya bishara za Mtume[saw] pia zilitanguka. Kama bishara yangu yoyote inapingwa hivyo, basi nijibuni hilo. Ikiwa mtanikadhibisha katika jambo hilo, basi si mtanikadhibisha mimi, bali mtakuwa wenye

---

[32] Na kama akiwa mkweli, yatawafikieni baadhi ya hayo anayowaonyeni. Al-Mu'min, 40:29 [Mwenezi]

kumkadhibisha Mwenyezi Mungu. Nasema kwa yakini kabisa kwamba suala hili limekubaliwa na Jumuiya nzima ya Ahli Sunna na dunia nzima kwamba kwa kunyenyekea, ahadi ya adhabu hutanguka. Je, mmesahau hata mfano wa Nabii Yunus[as]. Ni sababu ipi iliyoifanya adhabu ya kaumu ya Nabii Yunus[as] kuondolewa. Tazameni Durre Manthur n.k., na ndani ya Biblia kuna kitabu cha Nabii Yona. Adhabu hiyo iliahidiwa kabisa, lakini watu wa Yunus, kwa kuona alama za adhabu, wakatubu na kurejea Kwake. Mwenyezi Mungu Akawasamehe na adhabu ikaondolewa. Huko Nabii Yunus[as] alikuwa akingojea adhabu katika siku iliyowekwa. Alikuwa akiwauliza watu; akamwuliza mkulima mmoja kwamba hali ya Ninawi ikoje? Akajibu, ni nzuri tu. Hapo Nabii Yunus[as] akaingiwa na huzuni nyingi na akasema:

لَنْ اَرْجِعَ اِلٰى قَوْمِى كَذَّابًا

Yaani, sitarejea kwa watu wangu nikiitwa mwongo. Sasa juu ya kuwepo kwa mfano huu na kuwepo kwa ushahidi wa Kurani Tukufu, kupinga bishara yangu iliyokuwa na sharti tokea mwanzo ni kinyume cha ucha-Mungu. Si alama ya mcha-Mungu kutamka neno bila kutafakari na kuwa tayari kukadhibisha.

Kisa cha Nabii Yunus[as] ni cha kutia uchungu mno na ni chenye kutoa somo nacho kimeandikwa ndani ya vitabu. Kisomeni kwa makini, hata akatupwa mtoni na kuingia tumboni mwa samaki; ndipo toba ikakubaliwa. Kwa nini

adhabu na kasirani hii ikamsibu Nabii Yunus[as]? Ni kwa sababu hakufikiri kwamba Mwenyezi Mungu Anaweza kutangua ahadi ya adhabu. Kwa nini basi ninyi mnafanya haraka kunihusu mimi na kwa kunikadhibisha mnawakadhibisha Manabii wote?

Kumbukeni kwamba jina la Mwenyezi Mungu ni Ghafur (Msamehevu), kwa nini basi Asiwasamehe wanaomrejea? Ni makosa ya aina hii ambayo yameingia katika Waislamu. Miongoni mwa makosa hayo ni kosa kukusu Jihadi pia. Nastaajabu kwamba nisemapo kuwa Jihadi ni haramu, basi hutoa macho yenye hasira, ilhali wenyewe wanaamini kwamba Hadithi kuhusu Mahdi Mwaga damu zina dosari. Sheikh Muhammad Husain wa Batala ameandika vijitabu juu ya mada hii na huo ndio uliokuwa msimamo wa Mian Nazir Husain wa Delhi. Hao kabisa hawazitambui kuwa sahihi. Kwa nini basi naitwa mwongo. Ukweli ndio huu kwamba kazi ya Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi ndiyo kwamba ataondoa vita vya kidini na ataishindisha Islam kwa kalamu, maombi na nguvu ya kiroho. Lakini ni masikitiko kwamba watu hawaelewi habari hii, kwa sababu hawaielekei dini jinsi wanavyoielekea dunia. Baada ya kujiingiza katika unajisi na uchafu wa dunia wanawezaje kuwa na tumaini kwamba yatawafungukia maarifa ya Kurani Tukufu. Humo mmeandikwa kwa uwazi kabisa:

لَا يَمَسُّهٗٓ اِلَّا الْمُطَهَّرُوْنَ [33]

---

[33] Hapana atakayeigusa ila waliotakasika.—Al-Waaqi'a, 56:80 [Mwenezi]

Sikilizeni kwa makini kwamba shabaha ya kuja kwangu ni nini? Shabaha na kusudi la ujaji wangu ni kuijadidisha Islam tu na kuisaidia. Msidhani kwamba nimekuja nifundishe sheria mpya au nitoe maagizo mapya, au kitabu kipya kitashuka. Hata kidogo. Kama mtu anadhani hivyo, naona huyo amepotea kabisa naye hana imani. Kwa ujaji wa Mtume[saw] sheria na unabii umekwisha. Sasa sheria yoyote mpya haiwezi kuja. Kurani Tukufu ni Khatamul-Kutub [mwisho wa vitabu]. Humo sasa hamna nafasi ya kupunguza au kuongeza hata yodi moja wala nukta moja. Naam, ni kweli kwamba baraka na neema za Mtume[saw] na matunda ya mafundisho na mwongozo wa Kurani Tukufu hayakumalizika, bali hupatikana katika kila zama, na kwa kuthibitisha neema na baraka hizo Mwenyezi Mungu Amenituma. Hali ya Islam iliyopo hivi sasa haifichikani. Imekubaliwa na wote kwamba Waislamu wanaendelea kudhoofika kwa kila jiha na kurudi nyuma na hali yao inazidi kuwa mbaya kwa kila jiha. Wana maneno matupu tu, matendo hamna na Islam imekuwa yatima. Katika hali hiyo Mwenyezi Mungu Amenituma ili kuisaidia na kuilinda. Na Amenituma sawa na ahadi Yake, kwa sababu Alisema:

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ [34]

[34] Hakika Sisi Tumetermsha mauidha na hakika Sisi ndio Tuyalindao. Al-Hijr, 15:10 [Mwenezi]

Kama si wakati huo wa kuisaidia na kuinusuru na kuilinda Islam, ni wakati gani mwingine tena? Sasa katika karne hii ya kumi na nne hali inakuwa ile ile iliyokuwa wakati wa [vita vya] Badri ambayo kuhusu hali hiyo Mwenyezi Mungu Anasema:

وَلَقَدْ نَصَرَكُمُ اللّٰهُ بِبَدْرٍ وَّ اَنْتُمْ اَذِلَّةٌ [35]

Kwa hakika ndani ya aya hii mlifichikana bishara moja, yaani katika karne ya kumi na nne Islam itakapodhoofika na kuishiwa nguvu, wakati huo Mwenyezi Mungu sambamba na ahadi ile ya kuilinda, Ataisaidia. Kwa nini basi mnastaajabu kwamba Yeye Alinusuru Islam? Mimi sisikitiki kwamba naitwa Dajjal na mwongo mkubwa na ninasingiziwa. Kwani ilikuwa lazima nitendewe kama walivyotendewa Mitume wa kabla yangu ili nami ningepata hadhi ya sunna ya zamani. Mimi kwa kweli sikupata sehemu ya hizo taabu na shida, lakini misiba na matatizo aliyokabili Kiongozi na Bwana wetu Mtume[saw] mfano wake haupatikani katika mnyororo wa Manabii. Kwa ajili ya Islam yeye alipata udhia ambao kalamu inashindwa kuuandika na ulimi kuueleza. Hii inaonyesha jinsi Mtume[saw] alivyokuwa Nabii mwenye shani kubwa na imara. Kama kusingekuwa na msaada wa Mwenyezi Mungu na nusura pamoja naye, basi hangeweza kuvumilia shida hizo kubwa kama mlima. Kama angelikuwa Nabii

[35] Na bila shaka Mwenyezi Mungu Aliwasaidieni katika (vita vya) Badri hali ninyi mlikuwa dhaifu.—Aali‘Imran, 3:124 [Mwenezi]

mwingine, angelishindwa. Lakini Islam aliyoeneza kwa shida na taabu, nisemeje juu ya hali yake ilivyo leo.

Islam ilikuwa na maana kwamba mtu ajipoteze katika mapenzi ya Mungu na utii Wake; na kama vile shingo ya mbuzi huwa mbele ya mchinja, vivyo hivyo Mwislamu ajitolee kwa utii wa Mwenyezi Mungu. Na shabaha yake ilikuwa kumwamini Mwenyezi Mungu kuwa Mmoja, Asiye na mshirika. Mtume[saw] alipotumwa, wakati huo Umoja wa Mungu ulikuwa umepotea na nchi hii ya Waarya pia ilijaa masanamu kama Pandit Diyanand S'arasvati pia alivyokiri. Katika hali hiyo na wakati huo ilikuwa lazima atumwe Mtume[saw]. Zama hizi pia zinafanana na zama hizo ambamo pamoja na ibada ya masanamu, ibada ya mwanadamu na udaharia pia umeenea, na shabaha hasa ya Islam na roho yake haikubaki. Kiini chake kilikuwa kujipoteza katika mapenzi ya Mungu tu na kuamini hakuna mwabudiwa minghairi Yake; na shabaha ni kwamba mtu amwelekee Mungu wala asiielekee dunia. Kwa shabaha hiyo Islam imegawa mafundisho yake katika sehemu mbili: Kwanza, haki za Mungu; pili, haki za watu. Haki ya Mungu ni kumfahamu kwamba ni lazima Atiiwe, na haki za watu ni kuhurumia viumbe wa Mungu. Si vizuri kumdhuru mtu kwa sababu ya hitilafu ya dini. Kumhurumia mtu na kumtendea vizuri ni kitu kimoja na hitilafu ya dini ni kitu kingine. Kundi la Waislamu waliofahamu vibaya maana ya Jihadi na kuielewa visivyo, wamehalalisha

kunyang'anya mali ya makafiri. Mimi pia wakanitolea fatuwa kwamba chukueni wake zao; ilhali mafundisho machafu ya aina hii hayakuwa ya Kiislamu. Hiyo ilikuwa dini iliyosafika na kutakasika. Tunaweza kutoa mfano wa Islam kwa baba anayetaka haki za ubaba na kadhalika anataka watoto wake wahurumiane wao kwa wao wala hataki wapigane. Islam inapotaka pasiwepo mshirika yeyote wa Mwenyezi Mungu, papo hapo yataka pia kwamba wanadamu wawe na upendo na umoja.

Thawabu zaidi katika sala ya jamaa inayopatikana, shabaha yake ni hii tu kwamba hiyo huleta umoja, na kwa kuleta umoja huo kivitendo, imeagizwa na kusisitizwa kwamba miguu iwekwe sawasawa na mstari unyoke na wasimame bega kwa bega. Hii inamaanisha kwamba hao wote ni kama mtu mmoja ili kwamba nuru za mmoja ziweze kupenya ndani ya mwingine na ubaguzi unaozalisha majivuno na ubinafsi usibaki.

Kumbukeni vizuri kwamba mtu ana nguvu ya kuzivutia nuru za mwingine. Halafu kwa ajili ya umoja huo kuna amri kwamba sala za kila siku zisaliwe katika msikiti wa mtaa na baada ya wiki katika msikiti wa mji na kisha baada ya mwaka wajumuike katika uwanja wa Idi; na Waislamu wa dunia nzima, mara moja kwa mwaka, wakusanyike katika Nyumba ya Mungu. Shabaha ya maagizo yote hayo ni huo huo umoja.

Mwenyezi Mungu Amezigawa haki katika sehemu mbili: Kwanza, haki za Mungu; pili, haki za watu. Hiyo

imeelezwa sana katika Kurani Tukufu. Mwenyezi Mungu Anasema mahali pamoja:

فَاذْكُرُوا اللّٰهَ كَذِكْرِكُمْ اٰبَآءَكُمْ اَوْ اَشَدَّ ذِكْرًا [36]

Yaani, Mkumbukeni Mwenyezi Mungu kama mnavyowakumbuka baba zenu bali Mkumbukeni zaidi. Humo mna madokezo mawili. Kwanza, kumkumbuka Mwenyezi Mungu kumefananishwa na kuwakumbuka baba. Humo mna siri hii kwamba mapenzi ya baba huwa ni mapenzi ya dhati na ya asili. Tazameni mtoto anapopigwa na mama, hata wakati huo pia hulia, 'mama, mama'. Ndiyo kusema kwamba ndani ya aya hii Mwenyezi Mungu Anamfundisha mtu kwamba awe na uhusiano wa mapenzi ya asili na Mwenyezi Mungu. Baada ya mapenzi haya kupatikana, kutii amri za Mwenyezi Mungu hupatikana kwenyewe. Hii ndiyo daraja ya kweli ya maarifa ambayo mtu anatakiwa kuifikia. Yaani ndani yake mapenzi ya dhati na ya asili kwa ajili ya Mwenyezi Mungu yazalike. Mahali pengine Anasema hivi:

اِنَّ اللّٰهَ يَاْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْاِحْسَانِ وَاِيْتَآئِ ذِى الْقُرْبٰى [37]

Katika aya hiyo madaraja matatu yameelezwa ambayo mwanadamu anatakiwa kuyapata. Daraja la kwanza ni la uadilifu. Na uadilifu ni kwamba mtu amfanyie mwenzake

---

[36] Al-Baqara, 2:201 [Mwenezi]
[37] Kwa hakika Mwenyezi Mungu Anaamuru uadilifu, na hisani, na kuwapa (watu kama uwapavyo) ndugu.—An-Nahl, 16:91 [Mwenezi]

wema kwa sababu amefanyiwa wema. Na ni wazi kwamba wema huo si wa hali ya juu. Bali daraja la chini kabisa ni, 'fanyeni uadilifu'. Na kama mkiendelea mbele zaidi, hapo ndipo mtaingia katika daraja la hisani, yaani kufanya wema bila ya kufanyiwa wema. Lakini atendaye vibaya atendewe wema; apigaye shavu moja ageuziwe na la pili, si sawa. Au tuseme kikawaida fundisho hili haliwezi kutekelezwa, asemavyo Sa'adi:

نکوئی بابداں کردن چناں است
کہ بد کردن برائے نیک مرداں [38]

Hivyo mafundisho ya hali ya juu iliyotoa Islam kuhusu mipaka ya kujilipiza kisasi, hakuna dini yoyote inayoweza kuleta mafundisho kama hayo, nayo ndiyo haya:

جَزٰٓؤُا سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا ۚ فَمَنْ عَفَا وَاَصْلَحَ فَاَجْرُهٗ عَلَى اللّٰهِ [39]

Yaani, malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa nao, na anayesamehe sharti msamaha ulete marekebisho [basi ujira wake ni juu ya Mwenyezi Mungu]. Islam imetoa fundisho la kusamehe kosa sharti shari isiongezeke kwa sababu ya kusamehe.

Ilmuradi, baada ya uadilifu daraja la pili ni la hisani; yaani kutendea wema bila ya kutendewa wema. Lakini kutendea huko wema kuna ubinafsi wa

---

[38] Kuwatendea wema waovu ni kama kuwatenda vibaya watu wema. [Mwenezi]

[39] Ash-Shura, 42:41 [Mwenezi]

aina fulani, kwani wakati mwingine mtu humsimbulia mwenzake hisani au wema huo. Kwa hiyo imetoa fundisho lililo bora zaidi nalo ni daraja la: اِيْتَآئِ ذِی الْقُرْبٰی [kuwapa watu kama uwapavyo ndugu]. Mama anaye-mtendea wema mtoto wake huwa si mwenye kutamani kutoka kwake malipo na zawadi na heshima. Wema anaomfanyia hufanya kutokana na mapenzi ya asili. Kama mfalme akimwamuru: Usimnyonyeshe na hata kama akifa kwa kughafilika kwako, hutapewa adhabu, bali utapewa zawadi, hata hivyo hatakuwa tayari kutii amri ya mfalme, bali atamtukana kwamba huyo ni adui wa watoto wangu. Sababu yake ndiyo hii kwamba yeye anatendea hivi kwa mapenzi ya dhati; hana shabaha yoyote katikati. Hili ni fundisho la hali ya juu litolewalo na Islam. Na aya hii inakusanya haki zote mbili—haki za Mungu na haki za watu. Kulingana na haki za Mungu, maana ya aya hii ni kwamba kwa kuzingatia uadilifu Mtiini Mwenyezi Mungu na kumwabudu Yeye Ambaye Amewaumbeni na Huwaleeni. Na yule ambaye katika utii wa Mungu anaendelea mbele zaidi, atii kwa kuzingatia hisani. Kwani Yu Mhisani na hakuna awezaye kuzihesabu hisani Zake. Na kwa vile kuzingatia sifa na khulka njema za mhisani, hukumbusha hisani zake, ndiyo sababu Mtume[saw] alisema kwamba maana ya hisani ni kwamba mtu amwabudu Mwenyezi Mungu kana kwamba anamwona au angalau Mwenyezi Mungu

Anamwona. Mpaka daraja hilo kunakuwa na pazia kwa mtu, lakini baada yake kuna daraja la tatu la اِيۡتَآئِ ذِى الۡقُرۡبٰى yaani mtu hupata mapenzi ya dhati ya Mwenyezi Mungu. Na kulingana na haki za watu nimekwisha eleza maana yake hapo awali, na pia nilieleza kwamba fundisho hili lililotolewa na Kurani Tukufu halikutolewa na kitabu kingine chochote, nalo ni kamili kiasi hiki kwamba hakuna awezaye kuleta mfano wake, yaani:

جَزٰٓؤُا سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثۡلُهَا ۚ فَمَنۡ عَفَا وَاَصۡلَحَ فَاَجۡرُهٗ عَلَى اللّٰهِ [40]

Humo sharti limewekwa kwa msamaha kwamba ulete suluhu. Dini ya Kiyahudi ilifundisha: ' Jicho kwa jicho' na 'Jino kwa jino'. Kwa sababu hii, tabia yao ya kujilipiza kisasi ilizidi sana na tabia hiyo ikaimarika kiasi hiki kwamba kama baba hakulipiza kisasi, basi likawa jukumu la watoto hadi wajukuu wake kulipiza kisasi. Kwa sababu hii, tabia yao ya inda ikaongezeka nao wakawa na mioyo migumu na wasio na huruma. Kinyume na fundisho hili, Wakristo wakafundisha kwamba akupigaye shavu moja, mgeuzie na la pili pia; na mtu akulazimishaye mwendo wa maili moja, nenda naye maili mbili n.k. Kasoro iliyomo ndani ya fundisho hili iko wazi kwamba haliwezi kutekelezwa. Na serikali za Kikristo zimethibitisha kwa vitendo kwamba fundisho hili lina kasoro. Je, Mkristo yeyote anaweza kuwa na moyo ya kwamba mtu

40 Malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa nao ; lakini anayesamehe na kusuluhisha, basi ujira wake ni juu ya Mwenyezi Mungu.
Ash-Shura, 42:41 [Mwenezi]

habithi akimpiga kofi amng'olee mbali jino naye amgeuzie shavu la pili kwamba naam, sasa ling'oe jino la pili pia. Habithi huyo atazidi kujasiri na kwa njia hii amani itachafuka. Basi tukubalije kwamba fundisho hili ni bora au linaweza kuwa sawa na matakwa ya Mwenyezi Mungu. Kama litekelezwe fundisho hilo, nchi yoyote haiwezi kuendelea vizuri. Adui akivamia nchi moja, akabidhiwe na ya pili pia, na afisa mmoja akikamatwa basi wengine kumi nao wakabidhiwe. Hizo ndizo dosari zilizomo ndani ya mafundisho hayo; na hilo halifai. Naam, inawezekana kwamba maagizo hayo yalikuwa kama sheria kwa zama maalum na zama hizo zilipopita mafundisho hayo hayakuwafaa watu wengine. Wayahudi waliishi utumwani kwa miaka mia nne, na kwa sababu ya maisha haya ya utumwa, mioyo yao ikawa migumu zaidi nao wakawa wenye chuki. Na ni jambo la kawaida kwamba anayekuwepo katika zama za mfalme fulani, khulka zake huwa kama za mfalme. Katika utawala wa Masingasinga watu wengi wakawa majambazi, lakini katika enzi ya Waingereza ustaarabu na elimu vinaenea na kila mtu anajitahidi kwa hivyo. Ilmuradi, kwa sababu ya kukaa chini ya utawala wa Firauni, wana wa Israeli walizidi katika dhuluma. Hivyo, katika zama za Taurati haja ya uadilifu ikawa kipaumbele, kwa sababu watu hao walikuwa hawana habari nao na walikuwa na tabia ya kikatili. Na walikuwa na yakini kwamba ni lazima malipo ya jino yawe kulivunja jino, na huu ni wajibu wetu. Kwa

sababu hiyo, Mwenyezi Mungu Akawafundisha kwamba habari hii haiishii uadilifu tu, bali hisani nayo ni ya lazima. Kwa sababu hii wakafundishwa kwa njia ya Nabii Isa[as] kwamba ukipigwa shavu moja mgeuzie na la pili. Na hilo lilipotiliwa mkazo sana mno, basi Mwenyezi Mungu, kwa njia ya Mtume[saw]. Akalikamilisha fundisho hilo. Yaani, malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa nao; lakini anayesamehe na msamaha ulete suluhu, basi ujira wake ni kwa Mwenyezi Mungu. Yeye Amefundisha kusamehe, lakini sharti suluhu ipatikane. Msamaha pasipofaa huleta madhara. Basi hapa ni lazima kutafakari kwamba kama kuna matumaini ya suluhu, basi inastahili tu kusamehe. Kwa mfano, kuna watumishi wawili. Mmoja ni mwungwana, mtiifu na mwenye kutakia heri, lakini kwa bahati anakosea. Hapo yafaa kumsamehe; haifai kumwadhibu. Lakini mwingine ni mwovu na mkorofi; kila siku huleta hasara na haachani na ukorofi wake. Kama huyo aachiliwe basi atazidi kuwa jasiri; huyo hana budi kuadhibiwa. Ilmuradi, tendeni sawa na hali ilivyo. Hili ni fundisho lililotolewa na Islam nalo ni fundisho kamili. Na baada yake hakuna fundisho au sheria nyingine inayoweza kuja. Mtume[saw] ni Khataman-Nabiyyin na Kurani Tukufu ni Khatamul-Kutub. Sasa hakuwezi kuwa na Kalima nyingine au Sala nyingine. Chohote alichosema Mtume[saw] au kutenda, na yote yaliyomo ndani ya Kurani Tukufu, wokovu hauwezi kupatikana kwa kuviacha hivyo. Atakayeviacha atakwenda Jahanamu. Hii

ndiyo imani na itikadi yetu. Lakini pamoja na hayo ikumbukwe kwamba kwa ajili ya umati huu mlango wa maongezi na Mwenyezi Mungu uko wazi na mlango huu kana kwamba ni ushahidi siku zote juu ya ukweli wa Kurani Tukufu na ukweli wa Mtume[saw]. Na kwa ajili yake Mwenyezi Mungu Amefundisha ndani ya Sura Al- Faatiha dua hii:

اِهۡدِنَا الصِّرَاطَ الۡمُسۡتَقِيۡمَ ۙ‏ صِرَاطَ الَّذِيۡنَ اَنۡعَمۡتَ عَلَيۡهِمۡ ۙ [41]

Dua Aliyofundisha kwa ajili ya kupata njia ya walioneemeshwa inaashiria kupata sifa bora za Manabii[as]. Na ni dhahiri kwamba ubora waliopewa Manabii[as] ulikuwa ni wa kupata maarifa ya Mungu na neema hii walipata kutokana na maongezi na Mwenyezi Mungu. Ninyi nanyi mnaitamani hiyo. Fikirini kwamba kwa kupata neema hiyo, Kurani Tukufu inaagiza kuomba dua hii, lakini matokeo ya agizo hilo hakuna au hata mtu mmoja katika umati huu hawezi kupata heshima hiyo na mlango huu umefungwa mpaka Kiyama. Niambieni je, hiyo itaonyesha fedheha ya Islam na Mtume[saw] au uzuri wake wowote? Nasema kwelikweli kwamba yule anayeamini hivyo anaiaibisha Islam wala hakuelewa kiini cha sheria. Miongoni mwa miradi ya Islam ni kwamba mtu asiseme kwa ulimi tu kwamba Mungu ni Mmoja, Asiye na mshirika, bali aitambue barabara. Na asiwe na imani tupu juu ya Pepo na Moto bali kwa hakika apate

[41] Utuongoze njia iliyonyoka, njia ya wale Uliowaneemesha. Al-Faatiha, 1: 6-7 [Mwenezi]

kujua hali za kipeponi katika maisha haya haya na ayaepuke madhambi yanayowakumba watu hayawani. Hiyo ilikuwa, na ndiyo shabaha kubwa ya binadamu na hiyo ni shabaha tukufu ambayo watu wengine hawawezi kuleta mithili yake katika dini yao wala kuonyesha mfano wake. Kusema anaweza kusema kila mtu, lakini ni nani awezaye kuleta mfano wake.

Nimewauliza Waarya na Wakristo kwamba toeni uthibitisho wowote wa kuwepo kwa Mungu mnayemwamini, lakini hawawezi kuleta chochote isipokuwa maneno matupu tu. Watu hao hawamjui Yule Mungu Ambaye Kurani Tukufu imeeleza habari Zake. Ili kumjua Yeye kulikuwa na njia moja tu ya maongezi na Mwenyezi Mungu iliyopambanua Islam katika dini nyingine. Lakini inasikitisha kwamba Waislamu hao, kwa sababu ya kunipinga wameikataa hata hiyo.

Kumbukeni kwa yakini kwamba uwezo wa kuepuka madhambi hupatikana mtu anapomwamini Mwenyezi Mungu kikamilifu. Hiyo ndiyo shabaha kubwa ya maisha ya mtu kwamba ajiokoe katika kucha za dhambi. Tazameni nyoka anayeonekana wa kupendeza, mtoto anaweza kutamani kumshika na hata kumkamata. Lakini mwenye akili ajuaye kwamba nyoka atamgonga na kumwua, hatajasiri hata kidogo kumkimbilia. Bali akijua kuwa ndani ya nyumba fulani kuna nyoka, basi humo pia hataingia. Vivyo hivyo sumu ambayo anaifahamu ni kitu cha kuua hatajasiri kuila. Halikadhalika, asipokuwa na

yakini kwamba dhambi ni sumu ya hatari hawezi kuepukana nayo. Yakini hii haiwezi kuzalika bila utambuzi. Sasa ni kitu gani kinachomfanya mtu ajasiri kutenda dhambi, ilhali anamwamini Mwenyezi Mungu na kuifahamu dhambi kuwa ni dhambi. Sababu yake si nyingine isipokuwa kwamba hana utambuzi wala busara inayozalisha tabia ya kuunguza dhambi. Kama hali hii haipatikani, basi itabidi kukiri kwamba, Mungu Apishe mbali, Islam haina shabaha yake ya asili. Lakini mimi nasema si hivyo. Shabaha hii Islam pekee inaitimiza kikamilifu, na njia yake ni moja tu: Maongezi na Mwenyezi Mungu. Kwani kwa hiyo yakini kamili juu ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu huzalika na hii inajulisha kwamba kwa hakika Mwenyezi Mungu Huchukia dhambi na Huadhibu. Dhambi ni sumu ambayo mwanzoni huwa ndogo, halafu huwa kubwa na hatimaye hufikisha kwenye kufuru.

Nasema kwa kupitia kwamba kila kaumu inahangaika kuepukana na dhambi. Kwa mfano, Waarya wamezusha kwamba hakuna njia nyingine ya kutakasika katika dhambi isipokuwa kuadhibiwa tu. Adhabu ya dhambi moja ni kuzaliwa mara laki kadha kwa sura ya viumbe mbali mbali. Mtu hawezi kutakasika mpaka apate kuzaliwa hivyo. Lakini hiyo ina matatizo mengi; lililo kubwa zaidi ni kwamba kama viumbe wote ni wenye dhambi, basi wokovu utakuwa lini? Na jambo la ajabu zaidi ni kwamba kwao imekubaliwa kwamba waliookoka, baada ya muda

fulani watatolewa katika nyumba ya wokovu. Basi wokovu huo wafaa nini? Wanapoulizwa mbona mnatoa baada ya wokovu? Ndipo baadhi yao wanasema kwamba ili kutoa nje, dhambi moja inabakizwa. Sasa semeni kwa kutafakari kwamba je, hii yaweza kuwa kazi ya Mungu Mweza? Tena kama kila nafsi inajiumba, Mungu si mwumbaji wake (Mungu Apishe mbali), basi ina haja gani kuwa chini yake?

Wakristo wana imani nyingine. Wamefikiria njia moja ya kujitakasa katika dhambi, nayo ndiyo kumwamini Nabii Isa[as] kuwa Mungu na mwana wa Mungu. Halafu muwe na yakini kwamba amebeba dhambi zetu na akalaaniwa kwa kusulubiwa. Mungu Apishe mbali. Sasa tafakarini kwamba kupata wokovu kuna uhusiano gani na njia hii? Ili kuokoa katika dhambi wamebuni dhambi nyingine kubwa zaidi kwamba mwanadamu amefanywa Mungu. Je, kunaweza kuwa na dhambi kubwa zaidi ya hiyo? Na baada ya kumfanya Mungu, papo hapo wakasema pia yu maluuni. Je, utovu wa adabu na kumvunjia Mwenyezi Mungu heshima zaidi ya hapo yawezekana? Mwenye kula na kunywa na mwenye haja nyingine akafanywa Mungu; ilhali ndani ya Taurati mmeandikwa kwamba kusiwe na Mungu mwingine, mbinguni wala ardhini. Tena fundisho hili liliandikwa juu ya milango na miimo; hilo likaachwa na kuzushwa mungu mpya asiyejulikana katika Taurati.

Nimemwuliza mwanazuoni wa Kiyahudi kwamba je, kwenu kuna habari ya Mungu atokaye tumboni mwa

Mariamu na kupigwa na Wayahudi. Hapo wanazuoni wa Kiyahudi wakanijibu kwamba huo ni uzushi tu. Katika Taurati habari ya Mungu wa aina hii haijulikani. Mungu wetu ni Yule Aliye Mungu wa Kurani Tukufu. Yaani jinsi Kurani Tukufu ilivyoeleza Umoja wa Mwenyezi Mungu, ndivyo tunavyoamini sawa na Taurati kwamba Mwenyezi Mungu ni Mmoja, Hana mshirika wala hatuwezi kumwamini mtu yeyote kuwa Mungu. Ni dhahiri kwamba kama Wayahudi wangekuwa wamepewa habari ya mungu ambaye angezaliwa kutoka tumboni mwa mwanamke, kwa nini wangempinga Nabii Isa[as] vikali sana? Hata kwamba wakamtundika msalabani na wakamkufurisha. Hii yaonyesha wazi kwamba hawakuwa tayari hata kidogo kuliamini jambo hili.

Ilmuradi, tiba ya kuondoa dhambi waliyopendekeza Wakristo ni tiba ambayo yenyewe inazalisha dhambi, nayo haina uhusiano wowote na kujiokoa katika dhambi. Wamependekeza dhambi kuwa tiba ya kuondoa dhambi ambayo haifai kwa hali yoyote. Watu hao ni marafiki wajinga wa nafsi zao na mfano wao ni kama wa yule nyani aliyemwua bwana wake. Kwa ajili ya kujikinga na kujiokoa katika dhambi wamependekeza dhambi ambayo haiwezi kusamehewa kwa hali yoyote, yaani wamefanya ushirikina na kumfanya mtu mnyonge kuwa Mungu. Ni furaha ilioje kwa Waislamu kwamba Mungu wao si Mungu wa aina hii ambaye anaweza kulaumiwa na kushambuliwa. Hao wanaamini nguvu Zake na kudra

Zake na wana yakini katika sifa Zake. Lakini wale waliomfanya mwanadamu kuwa Mungu au walizikataa kudra Zake, kwao kuwepo na kutokuwepo kwa Mungu ni sawa. Kwa mfano, Waarya wanaamini kwamba kila chembe imejiumba yenyewe na Yeye Hakuumba chochote. Sasa hebu semeni kama Mungu si Mwumbaji wa chembe basi kuna haja gani ya Mungu kwa ajili ya kuwepo kwa hizo. Kama nguvu zipo tu zenyewe zikiwa na uwezo wa kujiunga na kujitenganisha, basi semeni kwa uadilifu hizo zina haja gani tena ya Mungu. Mimi naona kwamba kati ya Waarya wenye imani hii na madaharia kuna tofauti kidogo sana. Sasa Islam pekee ndiyo dini iliyokamilika na iliyo hai na wakati umewadia wa kudhihiri tena utukufu na shani ya Islam, nami nimekuja kwa shabaha hiyo.

Waislamu wanatakiwa wazithamini nuru na baraka zinazoteremka wakati huu kutoka mbinguni na wamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba wamesaidiwa katika wakati unaofaa. Na Mwenyezi Mungu sawa na ahadi Yake Amewanusuru katika wakati wa msiba huu. Lakini kama hawataithamini neema hii ya Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi Mungu Hatawajali kitu. Yeye Atatekeleza kazi Yake, lakini juu yao itakuwa masikitiko.

Mimi nasema kwa nguvu sana na yakini kamili na busara kwamba Mwenyezi Mungu Amekusudia kuzifuta dini nyingine na kuipa Islam ushindi na nguvu. Sasa hakuna mkono wowote wala nguvu inayoweza

kupambana na kusudio la Mwenyezi Mungu. Yeye ni:

فَعَّالٌ لِّمَا يُرِيْدُ [42]

Enyi Waislamu, kumbukeni kwamba Mwenyezi Mungu kwa njia yangu Amewapeni habari hii, nami nimefikisha ujumbe wangu. Sasa kuusikiliza au kutokusikiliza ni hiari yenu. Ni kweli kwamba Nabii Isa[as] amekwisha fariki, nami nasema kwa kuapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba yule aliyeahidiwa kuja ndiye mimi. Pia ni kweli kabisa kwamba uhai wa Islam umo katika kifo cha Nabii Isa[as].

Ikiwa mtalitafakari suala hili, basi mtatambua kwamba hilo ndilo suala litakalofutilia mbali dini ya Kikristo. Hili ni boriti kubwa kabisa la dini ya Kikristo ambalo jengo la dini hii linalitegemea. Liacheni lianguke. Jambo hili lingetatuliwa kwa urahisi sana kama wapinzani wangu wangekuwa na ucha-Mungu na hofu Yake. Lakini tajeni jina la mtu mmoja tu ambaye akiacha unyama wake alinijia na kutaka kupata uhakika. Hali yao ni kwamba walitajapo tu jina langu povu huanza kutoka vinywani mwao, nao huanza kutukana. Je, mtu aweza kuipata haki kwa njia hii?

Mimi natoa aya za Kurani Tukufu na Hadithi za Mtume[saw] na Ijmai ya masahaba[ra]. Lakini hao hawasikilizi maneno hayo bali wanapiga kelele: Kafiri huyu, Dajjal! Ninasema kwa uwazi kabisa kwamba thibitisheni kutoka katika Kurani Tukufu kwamba Nabii Isa[as] alienda

---

42 Atendaye Apendavyo.—Al-Buruj, 85:17 [Mwenezi]

mbinguni akiwa hai; leteni dalili yoyote kinyume na Mtume[saw] kumwona [katika Mira'aj] au onyesheni kilicho kinyume na Ijmai ya kwanza iliyofanyika wakati wa Abu Bakr[ra] ambapo Mtume[saw] alifariki, lakini hatupati jawabu. Isitoshe, baadhi ya watu wanapiga makelele kwamba ikiwa Masihi ajaye si yule yule Masihi bin Mariamu, Nabii wa Kiisraeli, kwa nini basi jina hilo amepewa yule anayekuja? Mimi ninasema kwamba upinzani huu ni wa kijinga namna gani! Jambo la ajabu ni kwamba wapinzani wana haki ya kuwapa wana wao majina ya Musa, Isa, Daudi, Ahmad, Ibrahimu na Ismaili, lakini kama Mwenyezi Mungu Akimpa mtu fulani jina la Isa hapo wapinga. Hapa jambo la kutafakari lilikuwa kwamba je, mjaji amekuja na ishara au la? Kama wangezikuta ishara hizo wasingejasiri kukataa. Lakini hawakujali ishara na misaada, bali waliposikia tu madai, wakasema: [43] اَنْتَ كَافِرٌ

Ni jambo la kawaida kwamba njia ya kuwatambua Manabii na Mitume wa Mwenyezi Mungu ni miujiza na ishara zao. Kama mtu akipewa na serikali mamlaka, hupewa alama fulani, vivyo hivyo kwa kuwatambua Mitume wa Mwenyezi Mungu pia kuna ishara. Nami nasisitiza kusema kwamba Mwenyezi Mungu kwa kunisaidia Amedhihirisha ishara, si moja, si mbili wala si mia mbili bali malaki, na hizo si ishara ambazo hakuna asiyezijua, bali malaki ya watu wamezishuhudia. Nami

---

[43] Wewe ni kafiri [Mwenezi]

naweza kusema kwamba hata katika mkutano huu pia mamia ya waliozishuhudia wanaweza kuwepo. Ishara zimedhihirika kwa ajili yangu toka mbinguni na ardhini pia.

Ishara zilizohusika na madai yangu ambazo zilitabiriwa mapema na Manabii wengine na Mtume[saw], pia zimetimia. Kwa mfano, katika hizo kuna ishara ya kupatwa jua na mwezi ambayo nyote mmeiona. Ilitabiriwa katika Hadithi Sahihi kwamba katika zama za Mahdi na Masihi jua na mwezi vitapatwa katika mwezi wa Ramadhani. Sasa semeni ishara hiyo imetimia au la? Kuna yeyote anayeweza kusema kuwa hakuiona ishara hii? Halikadhalika, ilitabiriwa kuwa katika zama hizo tauni itaenea na itakuwa kali kiasi hiki kwamba kati ya watu kumi, saba watakufa. Sasa semeni ishara ya tauni ilidhihirika au la?

Tena, pia iliandikwa kwamba katika zama hizo njia mpya ya kusafiria itavumbuliwa itakayosababisha ngamia kuachwa. Je, kwa kuanzishwa garimoshi ishara hii haijatimia? Nihesabu mpaka wapi; ni mlolongo mrefu wa ishara. Sasa fikirini kwamba mimi mwenye kudai nimeitwa Dajjal na mwongo, basi ni ajabu gani kwamba ishara zote hizo zimetimia kwa ajili yangu mimi niliye mwongo? Na kama ajaye ni mwingine basi ameachiwa nini? Fanyeni uadilifu na Mwogopeni Mwenyezi Mungu. Je, Mwenyezi Mungu Humsaidia mwongo hivyo? Ni la ajabu kwamba kila aliyekuja kupambana nami alishindwa wala hakufanikiwa, lakini katika kila balaa na msiba

ambamo wapinzani walinitia, nikatoka salama u salimini na kufanikiwa. Sasa, aseme yeyote kwa kuapa kwamba waongo wanatendewa namna hii?

Ninalazimika kusema kwa masikitiko kwamba wana shida gani masheikh hao wenye rai za kunipinga. Kwa nini hawasomi Kurani Tukufu na Hadithi kwa makini. Je, hawajui kwamba viongozi waliotangulia wa umati huu wote walikuwa wakieleza ujaji wa Masihi Aliyeahidiwa kutokea katika karne ya kumi na nne na kashfi za wote wenye kuona kashfi zinaishia hapa. Ndani ya kitabu cha Hujajul-Karamah imeandikwa kwa uwazi kwamba karne ya kumi na nne haitapita [pasipo Masihi kutokea]. Hao ndio watu waliokuwa wakipanda juu ya mimbari na kueleza kwamba hata wanyama wameomba kujikinga katika karne ya kumi na tatu na kwamba karne ya kumi na nne itakuwa yenye baraka. Lakini imekuwaje kwamba karne ya kumi na nne ambamo Imam Aliyeahidiwa alitakiwa kufika, badala ya mkweli akaja mwongo na maelfu kwa malaki ya ishara zimedhihirika kumsadikisha na pia Mwenyezi Mungu Akamsaidia yeye tu katika kila uwanja na kila mapambano. Yafikirini mambo hayo, kisha mtoe jawabu. Kutamka neno kwa midomo ni rahisi, lakini kusema kwa hofu ya Mungu ni vigumu.

Zaidi ya hayo, jambo hili pia lafaa kuzingatiwa kwamba Mwenyezi Mungu Hampi mzushi na mwongo muhula mrefu hata ampite Mtume[saw]. Umri wangu ni miaka 67, na tangu nitumwe sasa ni zaidi ya miaka 23.

Kama ningekuwa mzushi na mwongo, Mwenyezi Mungu Asingenipatia muda mrefu kiasi hiki. Baadhi ya watu pia wanasema kuwa kuja kwako kumefaa nini? Kumbukeni, shabaha za ujaji wangu ni mbili: Kwanza ni kwamba wakati huu ambapo dini nyingine zimeishinda Islam kana kwamba zinaendelea kuitafuna, na Islam imekuwa nyonge sana na kama mtoto yatima. Hivyo, Mwenyezi Mungu Amenituma wakati huu ili nilinde Islam katika mashambulio ya dini batili na nitoe dalili zenye nguvu za Islam na thibitisho za kweli zake. Na thibitisho hizo, zaidi ya dalili za kielimu, ni zile nuru na baraka za kimbinguni ambazo hudhihirika daima kuisaidia Islam. Wakati huu kama mtasoma taarifa za mapadre, itajulikana kwamba wanatumia njia gani kuipinga Islam na nakala nyingi namna gani za kila gazeti lao zinatolewa. Katika hali hii ilikuwa ni lazima Islam ishindishwe. Basi kwa sababu hiyo, Mwenyezi Mungu Amenituma, nami nasema kwa yakini kwamba ushindi wa Islam utapatikana na alama zake zimekwisha dhihirika. Naam, hili ni jambo la kweli kwamba kwa ajili ya ushindi huu hakuna haja ya upanga na bunduki, wala Mwenyezi Mungu Hakunituma na silaha. Mtu anayedhania hivyo wakati huu, ndiye rafiki mjinga wa Islam. Shabaha ya dini ni kuishinda mioyo na shabaha hii haipatikani kwa upanga. Kuhusu upanga alionyanyua Mtume[saw], nimekwisha eleza mara nyingi kwamba ulikuwa kwa ajili ya kujilinda na kujikinga tu, na huo pia wakati dhuluma za wapinzani na makafiri

zilipovuka mipaka na ardhi ikawa nyekundu kwa damu ya Waislamu wanyonge. Ilmuradi, shabaha ya kuja kwangu ndiyo kwamba Islam ipate ushindi juu ya dini nyingine.

Shabaha ya pili ni kwamba watu wasemao kuwa sisi tunasali na tunafanya hivi na vile; haya ni maneno matupu. Hiyo inahitaji kwamba izalike hali ndani ya mtu iliyo kiini na asili ya Islam. Mimi nafahamu kwamba mtu hawezi kuwa mwaminio na Mwislamu mpaka ajipatie sifa za Abu Bakr, Umar, Uthman na Ali, Mungu Awaridhie wote. Hao hawakuipenda dunia, bali walijitolea wakfu maisha yao katika njia ya Mwenyezi Mungu. Lakini sasa bidii zote ni kwa ajili ya dunia tu. Watu wamezama sana katika mambo ya dunia hata kwamba hawakumwachia Mwenyezi Mungu nafasi. Biashara ni kwa ajili ya dunia; jengo ni kwa ajili ya dunia, bali hata sala na saumu, zikitekelezwa, ni kwa ajili ya dunia. Yote yafanywa kwa kupata ukaribu na watu wa kidunia, lakini dini haitiwi maanani. Sasa kila mtu anaweza kufahamu kwamba je, shabaha ya kukiri na kukubali Islam ni hiyo tu iliyofikiriwa, au shabaha yake ni tukufu zaidi? Ninavyojua mimi ni kwamba mwaminio hutakaswa na hupata sifa za Malaika. Kadiri anavyozidi kumkurubia Mwenyezi Mungu, ndivyo anavyosikia maneno ya Mwenyezi Mungu na kwayo hupata utulivu. Sasa kila mmoja wenu afikirie moyoni mwake kuwa je, amelipata daraja hili? Nasema kwelikweli kwamba ninyi mmetosheka na ganda tu ilhali hili si kitu. Basi jinsi ilivyo

kazi yangu kuzuia mashambulizi ya wasio Waislamu, ndivyo ilivyo kazi yangu kuzalisha ndani ya Waislamu hakika na roho ya Islam. Lile sanamu la dunia lililoheshimika mioyoni mwa Waislamu badala ya Mwenyezi Mungu, matamanio na matumaini yake yametiwa humo, mashtaka na suluhu vyote ni kwa ajili ya dunia, hilo sanamu nataka livunjiliwe mbali kabisa na adhama na utukufu wa Mwenyezi Mungu uimarike mioyoni mwao na mti wa imani utoe matunda mapya mapya. Wakati huu ni sura ya mti tu, si mti wenyewe, kwani kuhusu mti wenyewe Alisema:

اَلَمْ تَرَ كَيْفَ ضَرَبَ اللّٰهُ مَثَلًا كَلِمَةً طَيِّبَةً
كَشَجَرَةٍ طَيِّبَةٍ اَصْلُهَا ثَابِتٌ وَّفَرْعُهَا
فِي السَّمَآءِ ﴿٢٥﴾ تُؤْتِيْٓ اُكُلَهَا كُلَّ حِيْنٍۭ بِاِذْنِ رَبِّهَا [44]

Yaani, je, hukuona jinsi Mwenyezi Mungu Alivyotoa mfano, yaani mfano wa dini kamilifu kwamba neno hili tukufu ni kama mti mtukufu ambao mzizi wake ni imara na matawi yake yafika mbinguni nao hutoa matunda yake kila wakati kwa amri ya Mola wake. اَصْلُهَا ثَابِتٌ Muradi wake ni kwamba kanuni zake za imani ziwe imara na ziwe zimehakikika nazo zifikie daraja la yakini kamili na dini hiyo idumu kutoa matunda yake kila wakati, na wakati wowote isiwe kama mti uliokauka. Lakini semeni je, hali hiyo ipo sasa? Watu wengi wanasema kwamba kuna haja

[44] Ibrahim, 14:25,26 [Mwenezi]

gani [ya Mtume]? Ni mjinga namna gani mgonjwa asemaye kwamba kuna haja gani ya tabibu? Ikiwa hamjali tabibu wala haoni haja naye, matokeo yake si mengine ila kuangamia? Hivi sasa Waislamu bila shaka wamo katika kundi la wasemao اَسْلَمْنَا [tumesilimu], lakini hawamo katika kundi la wasemao اٰمَنَّا [tumeamini]. Na hali hiyo ya 'Tumeamini' huwa wakati wanapokuwa na nuru pamoja nao.

Ilmuradi, hayo ndiyo mambo ambayo kwayo nimetumwa. Hivyo, msifanye haraka kunikadhibisha, bali Mwogopeni Mwenyezi Mungu na kutubu, kwani akili ya mwenye kutubu huwa nyepesi. Ishara ya tauni ni ishara ya hatari sana na ufunuo Alionifunulia Mwenyezi Mungu kuihusu ni huu:

اِنَّ اللّٰهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتّٰى يُغَيِّرُوْا مَا بِاَنْفُسِهِمْ

Haya ni maneno ya Mwenyezi Mungu, na laana iko juu ya yule amzuliaye Mwenyezi Mungu uwongo. Mwenyezi Mungu Anasema kwamba nia Yangu itabadilika wakati mioyo itakapobadilika. Basi Mcheni Mwenyezi Mungu na kuiogopa ghadhabu Yake. Hakuna yeyote awezaye kuchukua dhima ya mwingine. Katika kesi ya kawaida pia watu wengi hawawezi kuonyesha uaminifu. Basi mwawezaje kuwategemea wengine huko Akhera ambayo kuihusu hiyo Mwenyezi Mungu Anasema:

يَوْمَ يَفِرُّ الْمَرْءُ مِنْ اَخِيْهِ [45]

[45] Siku ambayo mtu atamkimbia nduguye.—'Abasa, 80:35 [Mwenezi]

Wapinzani waliwajibikiwa kuwa na dhana njema na kutekeleza agizo la:

لَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهٖ عِلْمٌ [46]

Lakini wakafanya haraka. Kumbukeni mataifa ya zamani yaliangamia vivi hivi. Mwenye akili ni yule ambaye hata akiisha pinga, anapojua kwamba alikosea, anaacha kupinga. Lakini jambo hili hupatikana kama ucha-Mungu upo. Kwa hakika wanaume ndio wanaokiri makosa yao. Huyu ndiye shujaa na ndiye anayependwa na Mwenyezi Mungu.

Zaidi ya hayo, sasa ningependa kusema kidogo kuhusu Qiyas. Ingawa aya za Kurani na Hadithi zinanisaidia, Ijmai ya masahaba[ra] pia yaniunga mkono, ishara na misaada ya Mungu hunisadikisha na haja za zama hudhihirisha ukweli wangu, lakini hata kwa njia ya Qiyas pia hoja inaweza kukamilika. Hivyo, inatakiwa kuona Qiyas inasemaje? Binadamu hawezi kuwa tayari hata kidogo kukiamini kitu kisichokuwa na mfano wake. Kwa mfano, kama aje mtu na kusema kwamba upepo umemchukua mtoto wako na kumpeleka mbinguni au mtoto amegeuka kuwa mbwa na kukimbia, je mtaamini maneno yake bila sababu ya kiakili na kuyachunguza? Kamwe. Ndiyo sababu Kurani Tukufu inasema:

فَسْـَٔلُوْٓا اَهْلَ الذِّكْرِ اِنْ كُنْتُمْ لَا تَعْلَمُوْنَ [47]

---

[46] Usifuate usiyo na elimu nayo.—Bani Isra'il, 17:37 [Mwenezi]

[47] Basi waulizeni wenye kumbukumbu ikiwa ninyi hamjui. An-Nahl, 16:44 [Mwenezi]

Sasa litafakarini suala la kifo cha Nabii Isa[as] na kuruka kwake mbinguni. Achilia mbali dalili kuhusu kifo chake, ni jambo lisilopingika kwamba makafiri walimwomba Mtume[saw] mwujiza wa kupaa mbinguni. Sasa Mtume[saw] ambaye kwa kila jiha alikuwa mkamilifu na mbora kuliko wote alipaswa apae mbinguni, lakini akajibu kwa kufunuliwa na Mwenyezi Mungu:

قُلْ سُبْحَانَ رَبِّيْ هَلْ كُنْتُ اِلَّا بَشَرًا رَّسُوْلًا [48]

Muradi wake ni kwamba, sema Mwenyezi Mungu Ameepukana na kufanya kinyume na ahadi Yake. Kwa kuwa Yeye Amemharimishia binadamu kwenda mbinguni na mwili wake, basi kama mimi nikienda nitakuwa mwongo. Sasa kama itikadi yenu hii ni sawa kwamba Nabii Isa[as] alienda mbinguni, hapo padre yeyote akitoa aya hii ampinge Mtume[saw] mtamjibuje? Basi kuna faida gani ya kuamini mambo ambayo hayana msingi ndani ya Kurani Tukufu. Kwa njia hii mtakuwa wenye kuiaibisha Islam na Mtume[saw].Tena ndani ya vitabu vya zamani pia hakuna mfano wa aina hii. Na si haramu kufanya 'Ijtihadi'[49] kutoka katika vitabu hivyo. Mwenyezi Mungu Anasema kumhusu Mtume[saw] :

---

[48] Bani Isra'il, 17:94 [Mwenezi]

[49] Kama jambo fulani halionekani wazi katika Kurani Tukufu wala Sunna ya Mtume [saw] mtaalumu anajitahidi kutafakari mwenyewe na kuamua, hiyo yaitwa Ijtihadi. [Mwenezi]

شَهِدَ شَاهِدٌ مِّنْۢ بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ [50]

Na kisha Kasema:

كَفٰى بِاللّٰهِ شَهِيْدًۢا بَيْنِيْ وَبَيْنَكُمْ ۙ وَمَنْ عِنْدَهٗ عِلْمُ الْكِتٰبِ [51]

Na vivyo hivyo Akasema:

يَعْرِفُوْنَهٗ كَمَا يَعْرِفُوْنَ اَبْنَآءَهُمْ [52]

Wakati Anapotoa hivyo [vitabu] kuhakikisha utume wa Mtume[saw] basi kwa nini tukaharimishwa kufanya 'Ijtihadi' kutokana na hivyo?

Sasa miongoni mwa vitabu hivyo kuna kitabu cha Nabii Malaki kilichomo ndani ya Biblia. Humo mmetolewa ahadi ya kufika Nabii Eliya mara ya pili kabla ya ujaji wa Masihi. Basi Masihi bin Mariamu alipofika, akaulizwa kuhusu ujaji wa Eliya mara ya pili sambamba na bishara hii ya Nabii Malaki. Lakini Masihi[as] alitoa uamuzi kwamba yule ajaye amekwisha kuja kwa sura ya Yohana.

Sasa uamuzi huu umekwisha tolewa na mahakama ya Nabii Isa[as] mwenyewe kwamba ujaji wa mara ya pili muradi wake ni nini? Hapo Yahya [Yohana] hakuitwa mfano wa Eliya bali akaitwa Eliya mwenyewe. Sasa Qiyas hii pia inaniunga mkono. Mimi natoa mfano, lakini wanaonikataa hawatoi mfano wowote. Baadhi ya watu wanaoshindwa

---

[50] Shahidi miongoni mwa wana wa Israeli alishuhudia.—Al-Ahqaf, 46:11 [Mwenezi]

[51] Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Shahidi baina yangu na baina yenu, na (pia) yule mwenye elimu ya Kitabu.—Ar-Ra‘d, 13:44 [Mwenezi]

[52] Wanamjua kama wanavyojua wana wao.—Al-Baqara, 2:147 [Mwenezi]

wanasema vitabu hivyo vimebadilishwa na kugeuzwa. Lakini ni masikitiko kwamba watu hao hawajui kwamba Mtume[saw] na masahaba zake walikuwa wanavitumia kwa hoja na wanazuoni wengi wamesema kwamba kuvibadilisha muradi wake ni kugeuza maana. [Imam] Bukhari pia alisema hayo. Zaidi ya hayo, Wayahudi na Wakristo ni maadui wakali sana; vitabu vyao ni tofauti. Wao [Wayahudi] hadi sasa wanaamini kwamba Eliya atakuja mara ya pili. Kama si tatizo hili, si wangemwamini Nabii Isa[as]? Nina kitabu cha mwanachuoni mmoja Myahudi ambamo yeye anaandika kwa nguvu kabisa na kusisitiza kwamba kama nitaulizwa [siku ya Kiyama], basi nitaweka mbele [ya Mungu] kitabu cha Nabii Malaki kwamba humo ahadi ya kuja Eliya mara ya pili ilitolewa.

Sasa tafakarini kama juu ya udhuru huu wote, malaki ya Wayahudi wamekuwa watu wa Jahanamu na wakawa nguruwe na manyani, je kwa kunipinga mimi udhuru huu utakuwa sawa kwamba humo [katika Hadithi] Masihi bin Mariamu ametajwa. Wayahudi waliweza kuwa na udhuru, kwani hawakuwa na mfano. Lakini sasa hakuna udhuru wowote uliobaki. Kifo cha Nabii Isa[as] kimethibitika kutokana na Kurani Tukufu na kimesadikishwa na Mtume[saw] kumwona [katika Mi'raaj]. Tena ndani ya Kurani Tukufu na Hadithi neno مِنْكُمْ limetumika. Kisha Mwenyezi Mungu Hakunituma mikono mitupu; maelfu kwa malaki ya ishara zimedhihirika kunisadikisha. Na hata sasa kama mtu anakaa pamoja nami kwa siku arobaini ataona ishara.

Ishara kumhusu Lekhram ni ishara kubwa sana. Wapumbavu wanasema eti mimi nilimwulisha. Kama upinzani huu ni sawa, basi ishara za aina hii hazitaaminika tena. Kesho itasemwa kwamba Khusro Parvez, Mungu Apishe mbali, pengine aliulishwa na Mtume[saw]. Kuleta upinzani wa aina hii si njia ya wenye kuona na kutambua ukweli.

Mwishwoe, nasema tena kwamba ishara zangu si kidogo. Zaidi ya watu laki moja ni mashahidi wa ishara zangu nao wako hai. Msifanye haraka kunikataa, waila baada ya kufa mtajibuje? Kumbukeni kwa yakini kwamba Mwenyezi Mungu Yupo na Huthibitisha mkweli kuwa mkweli na mwongo kuwa mwongo.

*[Gazeti la Badr, 20 Desemba 1906 uk. 4 hadi 18]*

# *FAHARISI*


| | |
|---|---|
| ***Abdul Hamid*** | ***29,30*** |
| ***Abu Bakr***[ra] | |
| *Mungu Akamjaalia nuru na busara* | *17* |
| *hotuba yake baada ya kifo cha Mtume* [saw] | *17, 18* |
| *akawaimarisha masahaba* | *20* |
| ***Adamu*** | ***9, 17*** |
| ***Ahli Sunna*** | ***39, 42*** |
| ***Ahmad***[as]***, Hadhrat Mirza Ghulam*** | |
| *ametoka kwa Mungu* | *37,38* |
| *ndiye aliyeahidiwa kuja* | *60* |
| *hakuleta sheria mpya* | *44* |
| *shabaha za ujaji wake* | *44, 59, 64, 65, 66* |
| *zilionyeshwa ishara niingi kwa ajili yake* | *12, 61, 62,63,71,72* |
| *kumsalia Mtume* [saw] | *27* |
| *akasaidiwa na Mungu* | *2, 4, 5,8,13,38,63* |
| *yu ishara hai ya misaada ya Mungu* | *4* |
| *akafunuliwa kwa lugha mbali mbali* | *6* |
| *shukrani kwa Mungu* | *1, 2,13* |
| *akaitwa kafiri, mwongo na Dajjal* | *1,2, 3, 7, 11, 14, 26,38.45,60,62* |
| *wafuasi wake kukataliwa kuzikwa katika mava ya Waislamu* | *15* |
| *kesi ya Karam Din* | *31* |
| *kesi ya mauaji dhidi yake* | *3, 28, 29, 30* |
| *kufanana na Nabii Isa* [as] | *32* |
| *kwa nini kaitwa Isa bin Mariamu* | *61* |
| ***Ali***[ra] | ***65*** |
| ***Amerika*** | |
| *Kupelekewa vitabu vya Hadhrat Ahmad* [as] | *37* |

***Amritsar*** *7*

***Badr*** ***45***

***Batala*** ***7, 43***

***Barahin-e-Ahmadiyya***

*kuenezwa na kusomwa sana* *6, 9*
*kusifiwa na Sheikh Muhammad Husain wa Batala* *7,9*

***Biblia***

*Mtume*[saw] *na masahaba kutumia kwa hoja* *70*
*kugeuzwa kwake* *71*

***Bishara***

*aina mbili* *39*
*ni mwujiza mkubwa* *11*
*tofauti baina yake na matakwa ya Mungu* *41*
*bishara za maonyo hutanguka* *39, 41,42*
*baadhi ya bishara huwa na siri* *11*

***Bukhara***

*kupelekewa Barahin-e-Ahmadiyya* *9*

***Bukhari***[rh] ***(Imam)*** ***71***

***Delhi*** ***13, 24, 43***

***Dhambi***

*ni sumu ya hatari* *55,56*
*njia ya kujitakasa katika dhambi* *55,56,57,58*

***Dini***

*shabaha ni kuishinda mioyo* *64*

***Diyanand S'arasvati*** ***46***

***Douglas, Kapteni***

*akasikiliza kesi dhidi ya Hadhrat Ahmad*[as] *28*
*akamwachilia Hadhrat Ahmad* [as] *30*
*hakimu mwadilifu* *29*
*akaonyesha ushujaa kuliko Pilato* *32*

***Dowie*** ***31***

***Dua***

*kiini cha ibada* *8*
*Mungu Huipokea* *7*

***Durre Manthur*** ***42***

***Eliya*** ***70, 71***

***Firauni*** ***10, 52***

***Hassan bin Thabit*** ***19***

***Hujajul Karama*** ***63***

***Ibrahimu** [as]* ***25,26***

***Ijmai*** ***14, 19, 26,60,61***

***Ijtihadi*** ***69,70***

***Isa bin Mariamu**[as]*

*mteule wa Mungu* *28*
*kifo chake* *19, 60, 71*
*Kurani Tukufu* *18, 25,69*
*Hadithi* *25, 26, 61*
*Ijmai ya masahaba* *14, 19,60,61*
*suala la kifo au uhai wake si*
*sharti ya kuingia katika Islam* *15*
*kifo chake ni kifo cha Ukristo* *22, 24*
*imani katika kifo hubatilisha itikadi*
*za Ukristo* *23*
*kifo chake njia ya ushindi wa Islam* *24*
*uhai wa Islam umo katika kifo chake* *60*
*uhai wake haukufanyiwa Ijmai* *26*
*hatari za imani katika uhai wake* *22,24*
*kufanana na Masihi Aliyeahidiwa* *32*
*ujaji wake mara ya pili kwa namna ya mfano* *26*

***Islam***

*maana yake* *46*
*shabaha zake* *46,47, 54*
*sehemu mbili za mafundisho* *46, 47*
*dini safi, kamili na iliyo hai* *47,59*
*ni njia ya wokovu* *34*
*huleta umoja wa wanadumu* *47*
*ilienezwa kwa mafundisho yake* *35*

*ahadi ya ushindi wake* *23,24*
*hali yake ya kisasa* *44, 46,64*

***Jihadi***

*kutokuelewa Jihadi* *43,46*
*shabaha za vita za Mtume*[saw] *33,34, 35, 36,64*
*Islam haikuenezwa kwa upanga* *33*

***Jumuiya Ahmadiyya***

*imeanzishwa na Mungu* *2, 27*
*hitilafu ya kimsingi* *13,14*
*itikadi zake* *14,15,16,53*
*ahadi ya ushindi* *8*
*maendeleo yake* *1,2,13*
*inasingiziwa kutangua Jihadi* *33*

***Kaaba (Nyumba ya Mungu)*** ***47***

***Karam Din*** ***31, 32***

***Karne ya kumi na nne*** ***45,63***

***Khusro Parvez*** ***72***

***Kurani Tukufu***

*Khatamul- Kutub (mwisho wa viabu)* *44, 53*
*haiwezi kubadilishwa* *44*
*baraka zake hupatikana katika kila zama* *44*
*hamna wokovu paisipo kuifuata* *53*
*aya zake* *7, 11, 12, 18, 19,20, 21,25,36,37,39,40,41, 43,44,45,48,49,51,54, 60,66,67,68,69,70*

***Le Marchand*** ***29,30***

***Lekhram*** ***71***

***Ludhiana*** ***1, 2, 6, 9, 13***

***Madina***

*Barahin-e-Ahmadiyya kupelekwa* *9*
*Mtume*[saw] *kufuatwa hadi Madina* *33*
*kaburi la Mtume*[saw] *16*

***Mahdi***

*ataondoa vita vya kidini na kuishuidisha Islam* *43*

| | |
|---|---|
| *Hadithi kumhusu Mahdi Mwaga damu* | *43* |
| ***Makka*** | ***9,10, 33*** |
| ***Malaki*** | ***70, 71*** |
| ***Mariamu*** | ***57*** |
| ***Martin Clark*** | ***28, 29*** |
| ***Masahaba*** | |
| *wapenzi wa Mtume saw* | *18* |
| *wakajitolea kwa Mungu* | *65* |
| *wakajitolea kwa Mtume saw* | *20* |
| *wakaudhiwa sana* | *3* |
| *huzuni yao juu ya kifo cha Mtume saw* | *17,18* |
| *imani yao katika kifo cha Nabii Isa as* | *19* |
| ***Masihi Aliyeahidiwa (pia tazameni 'Ahmad')*** | |
| *Hadhrat Ahmad as ndiye Masihi ajaye* | *60* |
| *ishara za ujaji* | *62* |
| *atotokea katika karne ya kumi na nne* | *63* |
| *atamwua Dajjal na kuvunja msalaba* | *24* |
| *ataondoa vita vya kidini na kuishindisha Islam* | *23,36,43* |
| ***Masufi*** | ***26*** |
| ***Maulidi*** | ***17*** |
| ***Miraaj*** | |
| *Mtume saw alimwona Nabii Isa as katika wafu* | *25, 26, 71* |
| ***Muhammad saw*** | |
| *Mtume Mkamilifu na Mbora kuliko wote* | *69* |
| *Khataman Nabiyyin* | *17,53* |
| *Mtume mwenye shani kubwa* | *45* |
| *Mtume saw Nabii aliye hai* | *35* |
| *Mtume Mkarimu na mwenye baraka* | *17* |
| *Mtume kwa dunia nzima* | *19,20* |
| *rehema kwa walimwengu wote* | *19* |
| *baraka zote huweza kupatikana kwa kumfuata yeye tu* | *16, 27* |
| *baraka zake ni za kudumu* | *44* |
| *akapata udhia mwingi kwa ajili ya Islam* | *45* |
| *akatumia upanga kwa kujikinga tu* | *34* |

*akaombwa kupanda mbinguni* *69*
*umri wake* *16*

***Muhammad Hasan*** ***9***

***Muhammad Husain wa Batala***

*akasoma pamoja na Hadhrat Ahmad* [as] *7*
*katembelea Qadian* *7*
*maoni yake kuhusu Barahin-e-Ahmadiyya* *7,9*
*mpinzani na adui mkali wa*
*Hadhrat Ahmad* [as] *3, 28*
*Vijitabu juu ya Jihadi* *43*

***Muhammad Umar (Munshi)*** ***9***

***Mungu***

*Msamehevu* *43*
*Mhisani* *50*
*Karimu* *39*
*Rahimu* *39*
*Hupokea maombi* *7*
*Huonyesha ishara kwa Mitume na kuwasaidia* *38*
*Huwaokoa Mitume na watumishi*
*Wake wa kweli* *31, 32*
*Huwadhihirishia Mitume siri Zake* *11*
*Hupambanua mkweli na mwongo* *4*
*Hampi mwongo muda mrefu* *63*
*Huchukia dhambi* *56*
*Kumkumbuka Mungu* *48*

***Musa*** [as] ***10, 12, 25,26***

***Naushirwan*** ***28***

***Nawwab Siddiq Hasan Khan*** ***24***

***Nazir Husain (Mian)*** ***43***

***Ninawi*** ***42***

***Pilato***

*Mfuasi wa Nabii Isa* [as] *32*
*Hakuonyesha ushujaa*
*alivyoonyesha Douglas* *32*

***Qadian*** ***5, 7***

***Qiyas*** ***14, 28,70***

***Ramadhani***

*mwezi wa kufungu saumu* *16*
*kupatwa kwa mwezi na jua*
*katika Ramadhani* *62*

***Sala***

*hekima ya sala ya jamaa* *47*

***Saadi*** ***49***

***Sadaka***

*desturi hii hupatikana katika kila kaumu* *40*
*huondoa balaa* *41*

***Simla*** ***28***

***Tauni*** ***62,67***

***Taurati*** ***52, 57,58***

***Ufunuo***

*huendelea* *54*
*ni njia ya kupata maarifa ya Mungu* *54, 55*
*baadhi ya funuo za Hadhrat Ahmad [as]* *5, 6, 31, 67*

***Ukristo***

*imani juu ya Mungu* *57,58*
*mafundisho yasiyoweza kutekelezwa* *51,52*
*wokovu* *58*
*kifo cha Nabii Isa [as] ni kifo cha Ukristo* *22*
*imani katika kifo cha Nabii Isa [as] ni pigo*
*kwa Ukristo* *23*

***Ulaya***

*majarida ya Hadhrat Ahamad [as]*
*kufika Ulaya* *37*

***Umar[ra]*** ***17,18,65***

***Umoja***

*Umoja wa Mungu* *46, 58*
*shabaha ya Sala na Haji ni kuleta umoja* *47*

***Utawala***

*utawala wa Firauni* *52*

*utawala wa Kirumi* 28
*utawala wa Masingasinga* 52
*utawala wa Waingereza* 52
*utawala wa Waingereza hupenda amani na kutoa uhuru wa kidini* 27
*hisani zake* 33
*ni bora kuliko utawala wa Kirumi* 28, 32

***Uthman*** ***65***

***Waarya***

*imani juu ya Mungu* 59
*hawana dalili ya kuwepo kwa Mungu* 55
*wana tofauti kidogo sana na madaharia* 59

***Waislamu***

*hali yao ya kisasa* 44,67

***Wakristo***

*Itikadi zao* 23,57
*hawana dalili ya kuwepo kwa Mungu* 55
*maadui wakali wa Wayahudi* 71

***Wayahudi***

*imani katika Umoja wa Mugnu* 58
*waliishi utumwani kwa miaka 400* 52
*walimpinga na kumkufurisha Nabii Isa* [as] 58
*maadui wakali wa Wakristo* 71
*bado wanamngoja Nabii Eliya* 71

***Yohana (Mbatizaji)*** ***70***

***Yunus***[as] ***42, 43***

***Yusuf***[as] ***25***